# Nipashe

Ijumaa Januari 31, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581938

www.ippmedia.com 0677 020 710 MWANGA WA JAMII

Nipashe digital

LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ

epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com




**AMORIM: RASHFORD ATAKIWA KUBADILIKA**

UKURASA 21

UKURASA 3

**Ofisi** za TRA zawaka moto kuanzia juu

UKURASA 5

**Mganga** kienyeji, wengine watatu kortini mashtaka ya kuiba watoto

UKURASA 19

**Kagame**, Ramaphosa watunishiana misuli kwa kinachojiri DRC

# Jengo la Kariakoo laibua yaliyofichwa

1. Uwezo wake tani 250, likabebeshwa tani 800
2. Maghala yamesheheni bidhaa za magendo
3. Wageni wachukua majukumu ya machinga
4. Jangwani kujengwa 'Kariakoo' nyingine
5. Soko lilichomwa moto kupoteza ushahidi
6. Ataja sababu tatu anaendelea kukopa

• **Ni** lililoporomoka Novemba 16, 2024; Samia abainisha ya uvunguni... *Ukurasa 2*



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

## Lissu aibukia mahakamani kumtetea Slaa UK. 3



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Tundu Lissu (kulia) akisalimiana na aliyekuwa Balozi, Dk. Wilbroad Slaa alipokwenda kuungana na jopo la Mawakili wanaomtetea katika kesi inayomkabili ya kuchapisha taarifa za uongo katika mitandao ya kijamii, katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Mwisho kutumia kuni na mkaa leo


UKURASA 14



**MICHEZO** **SIMBA: TUTAIZIMA TABORA UNITED** UK.24

**MAONI,** UK.6

# Jengo la Kariakoo laibua yaliyofichwa




**Restuta James na Sajini Hamisi**

KUPOROMOKA kwa jengo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam kumeibua 'madudu' mengi yaliyokuwa yamefichika, ukiwamo udanganyifu kwenye maghala ya kuhifadhi mizigo na chanzo cha kuungua kwa Soko Kuu la Kariakoo.

Vilevile, uchunguzi wa tukio hilo umebaini mambo mengine ya ziada yakijumuisha ongezeko la wageni wanaofanya kazi za wazawa, shehena za magendo katika maghala ya Kariakoo na msongamano wa machinga kwenye barabara, hata kulazimu serikali kutangaza mpango wa kujenga Kariakoo mpya kwenye eneo la Jangwani.

Rais Samia Suluhu Hassan alitaja 'madudu' hayo jana Ikulu, jijini Dar es Salaam alipokutana na kula chakula cha mchana na watu walioshiriki uokoaji kwenye jengo la ghorofa lililoporomoka Kariakoo mnamo Novemba 16, 2024.

Alisema wingi wa mizigo kwenye jengo lililoporomoka ulichangia ajali hiyo kwa kuwa lilikuwa na uwezo wa kubeba tani 250, lakini lilikutwa na tani 850 za mzigo.

Rais Samia alisema taarifa ya awali kutoka kamati iliyochunguza jengo lililoporomoka, imebaini pia udanganyifu kwenye maghala ya kuhifadhi mizigo.

"Tumepata somo la jinsi biashara inavyoendeshwa pale Kariakoo. Tumeelezwa hapa kwamba jengo lile lilikuwa na uwezo wa kuchukua tani 250 za mzigo, lakini tani zilizokuwepo pale ni 850. Kwa hiyo kwa vyovyote vile lisingeweza kubeba. Hili ni jengo moja, nina hakika majengo mengi yaliyoko Kariakoo yako katika mfumo huu.

"Ambalo mimi niliona kwa harakaharaka na pengine ndilo kwa wakati ule lilileta mzozo wa wafanyabiashara wa Kariakoo, ni mali iliyofichwa mle ndani na pengine bila kulipiwa kodi.

"Sasa jengo lile limetufunulia tu mambo mengi. Sidhani kama tani zile 800 zililipiwa kodi na ndiyo maana TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) ilipeleka watu kuangalia maghala eneo la Kariakoo. Hili ni somo lingine ambalo tumelipata," alisema.

Rais aliielekeza TRA kuweka mazingira sawa ya ulipaji kodi kwa wafanyabiashara wote, ili kuweka mazingira ya haki ya ufanyaji biashara.

### SOKO JANGWANI

Kukiwa na maombi ya uongozi wa Klabu ya Yanga kujenga uwanja wa kisasa Jangwani, Rais Samia alisema serikali inakusudia kujenga soko kubwa na la kisasa kwenye eneo hilo. Litatumiwa na machinga, hivyo kupokea kilio cha wafanyabiashara kuwa barabara nyingi za Kariakoo zimevamiwa na machinga.

Alisema serikali inataka biashara zifanyike kwa saa 24 Kariakoo, hivyo ulinzi na miundombinu ya barabara inapaswa kuwa wazi na kupitika wakati wote.

"Wafanyabiashara ndogo wameziba njia na kujenga maduka barabarani. Tume wameliona hili, niwaombe tutakapokuja kutekeleza mapendekezo ya tume, mshirikiane nasi. Dar es Salaam tuna mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu (DMDP), ambao kati ya fedha zake, tumejipanga kujenga soko lingine kubwa na zuri kama la Kariakoo, maeneo ya Jangwani.

"Kwa hiyo, ni maoni yetu kwamba baadhi ya wafanyabiashara, wanangu machinga tutawahamisha tuwapeleke kwenye soko lile la Jangwani, wakafanye biashara zao kule kwa nafasi na kwa vizuri," alisema.

### MOTO KARIAKOO

Rais Samia pia alitaja chanzo cha kuungua Soko Kuu la Kariakoo Julai 10, 2021 ni njama zilizolenga kupoteza ushahidi wa kilichokuwa kinaendelea sokoni huko.

"Nilikuja Kariakoo na baada ya kuondoka tu, siku iliyofuata mkalitia moto. Baada ya kuzisema changamoto za uongozi uliokuwapo na mambo yaliyokuwa yanafanyika katika soko na kuvitaka vyombo vinavyohusika kufanya uchunguzi ndani ya soko, ili kupoteza ushahidi mkalichoma moto, lakini kwa ujasiri nikaamua kulijenga tena," alisema.

Alisema serikali imejifunza mambo manne baada ya kuporomoka kwa jengo, ikiwa ni pamoja na utanuzi wa majengo Kariakoo unaofanywa kwa msingi wa awali badala ya kujenga upya kulingana na ukubwa wa jengo.

"Tunarefusha juu, tunachimba chini, lakini kwa msingi uleule wa mwanzo. Hii ni hatari," alisema Rais na kusisitiza kuwa kuepusha hasara ya mali na maisha ya wananchi, serikali itaimarisha usimamizi wakati wote wa ujenzi.

### MPANGO UJAO

Alisema katika mipango ya baadaye, katika kukabiliana na maafa, serikali itanunua vifaa na rasilimali kusaidia uokoaji ili kukabiliana na maafa kwa ufanisi. Alisema vifaa vingi vya uokoaji vilivyotumika Kariakoo, vilikuwa vya sekta binafsi ambavyo serikali ilipaswa kuwa navyo.

Alisema serikali pia itaimarisha mifumo ya maafa na kuzijengea uwezo timu za usimamizi wa maafa za mikoa na wilaya, ili ziwe tayari kuyakabili yanapotokea.

"Tutahakikisha viwango vya ubora vya ujenzi vinazingatiwa ipasavyo na taratibu za ukaguzi wa majengo zinaimarishwa. Sheria za ujenzi zinafuatwa na rasilimali za kiufundi zinapatikana kwa ajili ya kusimamia sekta hiyo muhimu," alisema Rais Samia.

### WAGENI MACHINGA

Rais Samia pia alimwelekeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Seleman Jafo, kuhakikisha biashara za wazawa hazifanywi na wageni.

"Kuna kipindi nilirushiwa 'clip' mgeni anapigana na mwenyeji Kariakoo, nikasema 'huyu ni machinga wameshindwana kwenye shughuli zao...' haiwezekani mgeni akawe machinga, vijana wetu watafanya biashara gani? Waziri wa Biashara simamia hili," aliagiza.

### SABABU ZA KUKOPA

Mkuu wa Nchi pia alitoa sababu za serikali yake kuendelea kukopa, akisisitiza ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, shule na hospitali.

"Asiyejua anasimama anasema 'hii serikali kazi kukopa tu', kwani tunakopa kwenda kununua sare za harusi? Tunakopa kujenga reli, barabara, shule, huduma za afya, kufanya Dar es Salaam na Dodoma kuwa miji mikubwa inayoheshimika, tunakopa kukuza hadhi ya nchi yetu. Hakuna anayeendelea kukopa, tunakopa kwa sababu," alisema.

Rais Samia aliwataka wafanyabiashara kulipa kodi stahiki ili nchi ipunguze kukopa na kuomba misaada, akisema "kila anayefanyabiashara akichangia kidogo kidogo, kile kiwango cha kukopa kitapungua. Tutaendesha mambo mengi, kwa fedha tunayokusanya ndani. Niwaombe sana, tukashirikiane kwenye hilo.

"Kodi hizi ni mnayaona yanayotokea ndani ya nchi. Tusipolipa kodi na kuacha wachache walipe na kubeba wengi wasiolipa kodi, hii ni hasara kubwa kwa taifa," alisema.

Rais alisema hivi sasa TRA inakusanya wastani wa Sh. trilioni tatu kwa mwezi na kwamba lengo ni kukusanya Sh. trilioni nne kwa mwezi miaka michache ijayo na ikiwezekana mwakani. Hilo litawezekana kama mzunguko wa ufanyaji biashara na uwekezaji utaongezeka.

Hata hivyo, alisema wafanyabiashara wengi wa kati na wadogo wanakimbia kulipa kodi.

Awali, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema kwenye uokoaji Kariakoo, ziliokolewa fedha na marobota ya nguo yenye uzito wa tani 850.

Alisema ziliokotwa Sh. milioni 112.8, Dola za Marekani 48,490, fedha za China Yuan 631 na Sh. 6,920 za Kenya. Fedha hizo zote zimeendelea kurejeshwa kwa wamiliki waliotambuliwa.

Alisema kamati ya kuchunguza jengo lililoporomoka pamoja na majengo mengine, tayari imekamilisha kazi na kuwasilisha kwake na kwamba iko tayari kwa ajili ya kuiwasilisha kwa Rais.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Severine Mushi, aliwasilisha maombi mawili kwa Rais Samia; usawa wa kikodi uwekwe kwa wafanyabiashara na kuwaondoa machinga barabarani ili biashara zifanyike kwa wepesi Kariakoo.

Katika tukio hilo la Novemba 16 mwaka jana, watu 31 walipoteza maisha na wengine 71 waokolewa na kutibiwa.

Manusura wa tukio hilo la Kariakoo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Jengo Lililoporomoka, Martilda Zela, alisema wafanyabiashara walipoteza mitaji. Hadi sasa hawajarejea kwenye hali yao ya awali.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@***

## HABARI KITAIFA

# Jengo la TRA lawaka moto Kariakoo

**Na Halfani Chusi**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limefanikiwa kuuzima moto uliokuwa ukiteketeza jengo la Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kariakoo, jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia tukio hilo jana, Mkurugenzi wa Idara ya Elimu kwa Mlipakodi, Richard Kayombo baada ya kufika eneo la tukio, alisema haijulikani moto huo ulianza kuwaka muda gani japo juhudi za uokozi zinaendelea.

Alisema Jeshi la Uokoji, magari ya Zimamoto yameshafika katika eneo hilo na shughuli ya kuuzima ilikuwa ikiendelea.

"Bado hatujabaini nini chanzo cha moto huu, na kwa sasa siwezi kusema chochote mpaka pale tutakapofanikiwa kuudhibiti kwa sababu vyombo vyote vya dola viko hapa," alisema Kayombo.

Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda, alisema janga hilo lilikuwa nje ya uwezo wao na kwamba watakaa na kutathmini chanzo na kuchukua hatua.

Alisema jengo lililoathirika zaidi ni ghorofa ya tano ambalo lilikuwa na baadhi ya nyaraka na ukumbi wa mikutano. "Tunafanya juhudi za haraka ili walipa kodi wasipate shida yoyote kutokana na janga hili, kwa sababu taarifa nyingi muhimu zilikuwa hazikai ghorofa hilo ambalo limeathiriwa na moto," alisema Mwenda.

Naibu Kamishna Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Goodluck Zelote, alisema walipopata taarifa ya ajali hiyo haraka walipeleka mitambo ya kuzima moto.

"Mpaka sasa operesheni inaendelea tumefanikiwa kuuzima moto, lakini tutatoa taarifa kamili baada ya kumalizika kabisa kwa shughuli hii," alisema Zelote.

Baadhi ya mashuhuda walisema walipoona moshi mkubwa unafuka katika ghorofa hilo, walitoa taarifa Jeshi la Zimamoto kwa ajili ya uokozi.

Jabiri Mtulya, alisema moto huo haujaleta madhara makubwa kwa sababu ya kuwapo kwa vifaa vya kisasa vya uokozi.

"Sidhani kama kuna aliyepata majeraha kwa sababu moto ulianza kidogo kidogo kwahiyo ilikuwa rahisi kwa wao kujiokoa," alisema.

Shuhuda mwingine, Fatma Abubakari, alisema hajui chanzo, lakini anahisi hitilafu ya umeme huku akilipongeza Jeshi la Zimamoto kwa uharaka na kufanikisha uokozi kabla madhara hayajawa makubwa.

Abeli Mgonja, alisema kwenye majira ya saa sita mchana jengo hilo lilianza kuwaka moto ulioambatana na moshi mzito.

"Tunashukuru kulikuwa na askari walikuwa doria wakaanza kuweka ulinzi, na kufanya taratibu za uokozi lakini kuna mmoja wa walinzi kampuni binafsi aliteguka mguu wakati tunahamisha vitu," alisema Mgonja.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba akigonga kengele kuashiria kuorodheshwa rasmi kwa Hatifungani ya Benki ya Azania-Bondi Yangu kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) mwishoni mwa wiki. Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Felix Maagi (kulia), Mkurugenzi Mkuu wa CMSA, Nicodemus Mukama (wa pili kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Dk. Esther Mang'enya (wa pili kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa DSE, Peter Nalitolela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lissu aibukia mahakamani kumtetea Slaa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Masjala Ndogo ya Dar es Salaam imeirudisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kesi ya mwanasiasa mkongwe Dk. Wilbroad Slaa , huku ikielekeza suala la dhamana ya mshtakiwa kupewa kipaumbele.

Kukiwa na agizo hilo la Mahakama Kuu, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu ajitosa kumtetea Dk. Slaa baada ya jana kujitambulisha mbele ya Jaji Arnold Kirekiano wa Mahakama Kuu Masjala Ndogo Dar es Salaam kwamba anamwakilisha mshtakiwa huyo.

Dhamana kwa mwanasiasa huyo ilizuiwa tangu Januari 10 mwaka huu alipofikishwa mahakamani, hivyo kuendelea kusota kwenye Gereza la Keko, Dar es Salaam.

Dk. Slaa alifungua kesi ya mapitio ya kesi yake katika Mahakama Kuu, akipinga mwenendo wa Mahakama ya Kisutu kuahirisha usikilizwaji dhamana yake kutokana na maombi ya kuipinga yaliyowasilishwa na upande wa mashtaka.

Maelekezo hayo yaliyotolewa jana na Jaji Arnold Kirekiano wa mahakama hiyo, aliyesema kuwa kesi ya msingi iko katika Mahakama ya Kisutu ambayo ndiyo ina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, hivyo kuamuru kesi irudishwe huko ili itolewe uamuzi kwa sababu ilishafikia kwenye uamuzi.

Jaji Kirekiano pia alieleza kuwa shauri namba 1637/2025 ni maombi yanayohusu zuio la dhamana lililotolewa na upande mashtaka Januari 10, 2025 katika shauri namba 993/2025 lililoko Mahakama ya Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Beda Nyaki.

Jaji Kirekiano alisema kuwa katika maombi hayo, mpeleka maombi alikuwa na hoja saba ambazo aliziwasilisha mahakamani huko kupitia jopo la mawakili wa utetezi.

Alisema kuwa katika hoja zilizowasilishwa na Wakili Hekima Mwasipu, alidai wanaomba mahakama ipitie jalada la shauri 1015/2025 liliko mbele ya Hakimu Nyaki kwa kuwa hana ujuzi kwenye kuliendesha.

Pia alidai mpeleka maombi wao alipelekwa kwenye Gereza la Keko kinyume cha sheria, pia walidai kuwa mwenendo wa uendeshwaji kesi hiyo, Januari 10 na 13, 2025 ulikuwa na mazingira ya uzembe na upendeleo ambao kimsingi ulifanya uhuru wa mpeleka maombi kubebwa na mahakama.

Aliendelea kudai kuwa mwenendo wa uendeshwaji shauri hilo kwa tarehe tajwa ulikuwa si sahihi, pia waliomba mahakama hiyo ieleze kuwa shauri lolote linalohusu uhuru wa mshtakiwa lipewe kipaumbele kuliko mashauri yoyote yale, pia walidai kuwa maofisa wa mahakama wameendesha mashauri kwa kukiuka kanuni.

Jaji alisema kuwa maombi hayo yalikuwa sawasawa mahakamani hapo na msingi wake mkubwa ni malalamiko dhidi ya maahirisho katika Mahakama ya Kisutu na alipitia hoja za pande zote mbili.

Pia alisema mpeleka maombi na mawakili wake walijikita katika hoja kwamba kuna ukiukwaji utoaji haki kwa mshitakiwa kwa kutopewa haki ya kupewa dhamana kwa kuwa shtaka lake linadhaminika.

Alisema anakubaliana na msingi wa hoja ya kwamba suala la utoaji haki katika shauri ni wajibu wa mahakama kama ilivyotolewa na mlalamikaji.

Alisema katika utaratibu wa kawaida, mahakama hiyo ilipaswa kuamua kuhusiana na hatma ya mshtakiwa, lakini Upande wa Jamhuri ulikuwa na jambo lingine na hapo ndipo walipofungua maombi kwa ajili ya kuzuia mshtakiwa kupewa dhamana.

Jaji alisema kwa hoja ya wakili wa mpeleka maombi ni kwamba maahirisho yaliyofanyika Januari 13 hadi 23, 2025 hayakuwa sawa kwa kuahirisha shauri la dhamana kwa hoja ya kuwa na mrundikano wa mashauri.

Alisema dhamana ya mshtakiwa ni suala la haki ambayo linaleta maana kwenye dhana ya kwamba kila mtu hana kosa hadi pale itakapothibitika kuwa ametenda kosa, hivyo mambo yanayohusiana na hoja ya dhamana yanapaswa kufanyika siku ya kwanza mshtakiwa atakapofikishwa mahakamani.

Alisema panakuwapo pingamizi dhidi ya dhamana, basi hilo ni pingamizi dhidi ya haki ambalo linagusa uhuru wa mtu binafsi na kama mahakama itapaswa kusubiri, jambo hilo linapaswa kuwa la dharura zaidi. Pia maahirisho ya Januari 13 hadi Januari 23, 2025 hayakuwa ya msingi.

Alisema anamini maelezo hayo yatasaidia kuweka viwango katika mashauri kama hayo kwa siku zijazo.

Alieleza kuwa maombi kwenye hoja ya pili ambayo msingi wake ulikuwa unamgusa hakimu mwenyewe yanayohusu na suala la umahiri wa hakimu mahakama, si mahala pake na kusisitiza kuwa kila shauri lina mahali pake.

"Mahakama imezingatia mwenendo huu lakini haina mamlaka ya kubatilisha uhalali wa hati hiyo ya mashtaka kwani suala hilo linatakiwa kushughulikiwa na mahakama husika ambayo ni Mahakama Kisutu katika hatua ya kwanza," alisema.

Alisema hoja ya kushawishi mahakama hiyo kutolea uamuzi suala ambalo linasubiri uamuzi katika mahakama nyingine ni kuleta mkanganyiko, hivyo alielekeza uamuzi wa hoja ya uhalali wa mashtaka na dhamana itolewe katika Mahakama Kisutu.

Dk. Slaa anashtakiwa kusambaza taarifa za uongo kupitia mtandao wa X.

**LISSU AJITOSA**

Jana Lissu alijitambulisha Mahakama Kuu kabla ya jaji kutoa uamuzi wa mashauri mawili yaliyofunguliwa na Dk. Slaa kwa kushirikiana na jopo la mawakili wake kwa wakipinga mwenendo wa kesi ya tuhuma za kusambaza taarifa za uongo iliyoko katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Kabla ya uamuzi huo kutolewa, Lissu akiwa kwenye benchi la mawakili wa utetezi, alisimama na kutambulisha jopo lote kwa sababu yeye ndiye alikuwa wakili mkuu (senior Advocate), akidai wote wanamwakilisha mshtakiwa.

Mawakili wengine wanaomwakilisha Dk. Slaa ni Peter Madeleka, Hekima Mwasipu, Sanga Melikiole, Sisty Aloyce, Edson Kiratu na Mwanaisha Mdeme.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MUTASINGWA SAULO KAIMUKILWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 163 DGY** aina ya **Toyota IST**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa ya Polisi:**

**PHQ/DAR/ILA/15925/2025**

MKOMBOZI COMMERCIAL BANK
a bank with integrity

## MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE DISEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa Dec-24 | Robo Mwaka ya /Kipindi Kilichopita Sep-24 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 7,604 | 6,087 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 13,864 | 16,747 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 50,818 | 55,177 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 12,608 | 5,839 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | 104 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 11 | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 15,297 | 13,886 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 162,767 | 156,695 |
| 12 | Mali Nyingine | 8,908 | 10,240 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 539 | 539 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 12,185 | 14,178 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **284,601** | **279,492** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 214,652 | 213,008 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | 6 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 5,291 | 7,158 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baad | 9 | 9 |
| 27 | Dhima Nyingine | 9,451 | 8,989 |
| 28 | Madeni | 13,700 | 7,268 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **243,103** | **236,438** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **41,498** | **43,054** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 23,555 | 23,555 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 5,423 | 7,476 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 3,435 | 3,435 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 10,260 | 9,763 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | (1,175) | (1,175) |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **41,498** | **43,054** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 4,241 | 3,573 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,428 | 8,650 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 3,180 | 2,560 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15% | 15% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4% | 5% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 77% | 75% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 58% | 57% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80% | 81% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1% | -1% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2% | 3% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA DISEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-12-2024 | Robo ya mwaka Linganishi mwaka uliopita 31-12-2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-12-2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-12-2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| 1 | Mapato ya Riba | 4,667 | 6,679 | 30,267 | 25,871 |
| 2 | Gharama za Riba | (2,574) | (1,876) | (7,654) | (8,109) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **2,092** | **4,803** | **22,613** | **17,762** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | **(487)** | 474 | **(2,290)** | (1,650) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **2,158** | **2,054** | **7,361** | **9,114** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,058 | 598 | 2,903 | 1,875 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,483 | 1,229 | 4,249 | 5,755 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | (383) | 227 | 208 | 1,484 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3,267)** | **(4,593)** | **(17,424)** | **(16,654)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,253) | (2,199) | (9,074) | (8,733) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,014) | (2,395) | (8,350) | (7,921) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **497** | **2,737** | **10,260** | **8,572** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | (942) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **497** | **2,737** | **10,260** | **7,630** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | (1,580) |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **497** | **2,737** | **10,260** | **6,050** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 198 | 185 | 198 | 185 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 21 | 116 | 436 | 324 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **13** | **13** | **13** | **13** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0% | 1% | 1% | 3% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1% | 3% | 6% | 28% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 48% | 53% | 50% | 48% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 4% | 9% | 9% | 10% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA DISEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31/12/2024 | Robo iliyopita 30/09/2024 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31/12/2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31/12/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za | | | | |
| | **Mapato/(Hasara) Halisi** | 497 | 3,639 | 10,260 | 8,572 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 487 | 786 | 2,289 | 2,466 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (6,072) | (13,090) | (28,506) | (19,223) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,644 | (1,143) | 7,255 | 22,818 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | | | | |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,405) | 569 | 2,099 | 583 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,328 | (607) | (2,411) | 649 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (416) | (679) | (1,664) | (349) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(3,937)** | **(10,525)** | **(10,678)** | **15,517** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (685) | (649) | (2,888) | (2,486) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na | - | - | - | (9,648) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | | | | - |
| | Mengineyo (bainisha) | 2,941 | (2,454) | (5,743) | 3,718 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **2,256** | **(3,103)** | **(8,630)** | **(8,416)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | (284) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 6,424 | 3,068 | 9,189 | 99 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | (5,744) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **6,424** | **3,068** | **9,189** | **(5,929)** |
| | | | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na | **4,742** | **(10,560)** | **(10,119)** | **1,171** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 23,101 | 33,661 | 37,962 | 36,791 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **27,843** | **23,101** | **27,843** | **37,962** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA DISEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa (2024)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **23,555** | **(735)** | **3,435** | **5,423** | **-** | **(440)** | **31,238** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | **10,260** | - | - | - | **10,260** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | | | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **23,555** | **(735)** | **13,695** | **5,423** | **-** | **(440)** | **41,498** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita (2023)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **23,555** | **(735)** | **(1,498)** | **2,726** | **-** | **1,140** | **25,188** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | **7,630** | - | - | - | **7,630** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | **(2,696)** | **2,696** | - | **(1,580)** | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | | | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | | **(1,580)** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **23,555** | **(735)** | **3,435** | **5,423** | **-** | **(440)** | **31,238** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA DISEMBA 2024

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

***Jina na Cheo***

Respige O. Kimati
**( Ofisa Mtendaji Mkuu)**

Vitalis Michael
(Mkuu Idara Ya Fedha)

Crispin Paul K.
**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)**
Imesainiwa: 24.01.2025

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

*Jina* ______________________

1.Gasper Casmir Njuu - Mwenyekiti wa Bodi

2. Uphoo Swai-Mjumbe wa Bodi
Imesainiwa: 24.01.2025

# CHADEMA Zanzibar yatangaza msimamo wake Uchaguzi Mkuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Zanzibar kimesema bila mabadiliko ya sheria na mifumo ya uchaguzi nchini, hakutakuwa na Uchaguzi Mkuu mwaka huu.

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Zanzibar, Said Mzee Miraji (pichani) amesema hawatakubali kuwa na sheria mbovu za uchaguzi na haiwezekani wakurugenzi wa halmashauri ambao ni wateule wa rais kuwa ni sehemu ya maofisa wa Tume ya Uchaguzi.

Alisema hayo visiwani Zanzibar jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye ofisi za chama hicho huko Rahaleo, mjini Zanzibar.

Makamu Mwenyekiti huyo alisema wanapozungumzia mabadiliko ya sheria ili kuwapo wagombea huru kwa nafasi ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na wabunge si jambo linalowanufaisha CHADEMA tu bali ni jambo litakalowanufaisha watanzania wote na wapenda demokrasia, hivyo wataendelea kusimamia hoja hiyo.

"Tunataka mgombea wa urais angalau apate asilimia 50 ya kura ndipo atangazwe kuwa mshindi. Haiwezekani mtu anapata chini ya kura ya asilimia 50 anatangazwa kuwa ndiye mshindi. Hii si haki, tunasema mtu huyo hajachaguliwa," alisema. Miraji alisema wanataka mfumo wa uchaguzi uwezeshe watu wawili walioongoza kupata kura nyingi, uchaguzi urudiwe ili kupata mshindi stahiki.

Alisema wako tayari Uchaguzi Mkuu usogezwe mbele ili sheria ya uchaguzi ifanyiwe marekebisho na kuwa na uchaguzi huru na haki.

Akizungumzia viti maalum, Makamu Mwenyekiti huyo alisema ili kuwapo usawa wa kijinsia, lazima kuwapo nafasi ya viti maalum vya wanawake na wanaume.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho kwa upande wa Zanzibar, Ali Ibrahim Juma alisema malengo ya chama hicho kwa upande wa Zanzibar ni kukiimarisha ili kushinda uchaguzi na kuchukua dola.

Alisema malengo hayo hayatofikiwa ikiwa wanachama wa chama hicho hawatakuwa kitu kimoja katika kujenga chama hicho, akisisitiza "chama imara cha siasa hujengwa na wafuasi wake imara".

Miraji pia aliwataka wanachama wa CHADEMA kuvunja makundi ya uchaguzi kwa kuwa uchaguzi ndani ya chama hicho umekwisha, hivyo ni vyema kuungana pamoja katika kuimarisha chama.




# Mganga wa kienyeji na wenzake kizimbani mashtaka kuiba watoto

**Na Hellen Mwango**

WATU wanne, akiwamo mganga wa kienyeji Abdulkarim Husein, maarufu Sharifu (42), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka matatu ya kula njama, kulaghai wazazi na kuiba watoto wawili.

Sharifu na wenzake walisomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Janeth Kaluyenda.

Mbali na Sharifu ambaye ni Mkazi wa Kijitonyama, washtakiwa wengine ni mkazi wa Manzese Ajentina, Hamida Mohamed (53), wakazi wa Chamwino, mkoani Morogoro, Hadija Kagombe 'Neema' na Aisha Selemani (43).

Upande wa Jamhuri ulidai katika shitaka la kwanza kuwa, Januari 11 mwaka huu, katika eneo la Tandika, Mtaa wa Kwale wilayani Temeke, Dar es Salaam, washtakiwa walikula njama ya kutenda kosa la kuiba watoto wawili.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku ya tukio na eneo la tukio la kwanza, washtakiwa wote kwa pamoja waliwalaghai wazazi na kufanikiwa kumuiba mtoto Mahad Mohamed.

Upande wa Jamhuri uldai katika shitaka la tatu kuwa siku na eneo la tukio la kwanza na la pili, washtakiwa wote kwa pamoja waliwalaghai wazazi na kufanikiwa kumwiba mtoto Husna Gulam.

Washtakiwa walikana mashtaka yote na wako nje kwa dhamana mpaka Februari 13 mwaka huu.


MKOMBOZI
COMMERCIAL BANK
a bank with integrity

## MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC

## MINIMUM DISCLOSER OF CHARGES AND TARIFFS

| Type of Charge | Item/Transaction | Recommended Standard Fees TZS | USD/EUR/GBP |
|---|---|---|---|
| Minimum Opening Balance | **Current account** | | |
| | Business (SME, Corp., Sole-Propriators) | 100,000 | 100 |
| | Community (Schools, Hospitals, NGO's, Institutions) | 20,000 | 100 |
| | Call | 50,000,000 | n/a |
| | Personal/Individual | 50,000 | 100 |
| | **Savings account** | | |
| | Business | 50,000 | 100 |
| | Diocese/Parish/Jumuiya | 20,000 | 100 |
| | Personal | 20,000 | 50 |
| | Intergrity | 50,000 | 100 |
| | Student | 5,000 | n/a |
| | Mwana | 15,000 | 100 |
| | Joint/Wanandoa | 30,000 | 100 |
| | Pensioners | 20,000 | n/a |
| | Salary | Free | Free |
| | Bishop | 50,000 | 100 |
| | Priest/ Nun | 20,000 | 100 |
| | Wajasiriamali | 16,000 | n/a |
| | VIKOBA/ Informal Groups | 20,000 | n/a |
| | MKCB Float/WAKALA | Free | n/a |
| Minimum Operating Balance | **Current account** | | |
| | Business (SME, Corp., Sole-Proprietors) | 100,000 | 100 |
| | Community (Schools, Hospitals, NGO's, Institutions) | 100,000 | 100 |
| | Call | 50,000,000 | n/a |
| | Personal/Individual | 50,000 | 100 |
| | **Savings account** | | |
| | Business | 50,000 | 50 |
| | Diocese/Parish/Jumuiya | 10,000 | 50 |
| | Personal | 10,000 | 50 |
| | Intergrity | 50,000 | 50 |
| | Student | - | n/a |
| | Mwana | 5,000 | 50 |
| | Joint/Wanandoa | 20,000 | 50 |
| | Pensioners | 5,000 | n/a |
| | Salary | - | - |
| | Bishop | 50,000 | 50 |
| | Priest/ Nun | 10,000 | 50 |
| | Wajasiriamali | 10,000 | n/a |
| | VIKOBA/ Informal Groups | 10,000 | n/a |
| | MKCB Float/WAKALA | - | n/a |
| Interest rate payable | **Current account** | | |
| | Business (SME, Corp., Sole-Propriators) | n/a | n/a |
| | Community (Schools, Hospitals, NGO's, Institutions) | n/a | n/a |
| | Call | Up to 4% | n/a |
| | Personal/Individual | n/a | n/a |
| | **Savings account** | | |
| | Business | n/a | n/a |
| | Diocese/Parish/Jumuiya | n/a | n/a |
| | Intergrity | Below 5mln - 2% Above 5mln - 5% | n/a |
| | Personal | Below 5mln - 0.5% Above 5mln - 2% | n/a |
| | Student | | n/a |
| | Mwana | | n/a |
| | Joint/Wanandoa | | n/a |
| | Wajasiriamali | | n/a |
| | Pensioners | n/a | n/a |
| | Salary | n/a | n/a |
| | Bishop | n/a | n/a |
| | Priest/ Nun | n/a | n/a |
| | VIKOBA/ Informal Groups | Below 5mln - 0.5% Above 5mln - 1% | n/a |

| Type of Charge | Item/Transaction | TZS | USD/EUR/GBP |
|---|---|---|---|
| Interest minimum earning balance | **Current account** | | |
| | Business (SME, Corp., Sole-Propriators) | n/a | n/a |
| | Community (Schools, Hospitals, NGO's, Institutions) | n/a | n/a |
| | Call | 50,000,000 | n/a |
| | Personal/Individual | n/a | n/a |
| | **Savings account** | | |
| | Business | n/a | n/a |
| | Diocese/Parish/Jumuiya | n/a | n/a |
| | Personal | 100,000 | n/a |
| | Intergrity | 500,000 | n/a |
| | Student | 100,000 | n/a |
| | Mwana | 100,000 | n/a |
| | Joint/Wanandoa | 100,000 | n/a |
| | Pensioners | n/a | n/a |
| | Salary | n/a | n/a |
| | Bishop | n/a | n/a |
| | Priest/ Nun | n/a | n/a |
| | Wajasiriamali | 100,000 | n/a |
| | VIKOBA/ Informal Groups | 100,000 | n/a |
| Monthly Maintainance Fee | **Current account** | | |
| | Business (SME, Corp., Sole-Propriators) | 18,000 | 10 |
| | Community (Schools, Hospitals, NGO's, Institutions) | Free | n/a |
| | Call | Free | n/a |
| | Personal/Individual | 12,000 | 10 |
| | **Savings account** | | |
| | Business | 10,000 | 10 |
| | Diocese/Parish/Jumuiya | Free | Free |
| | Personal | 3,000 | 3 |
| | Intergrity | Free | Free |
| | Student | Free | n/a |
| | Mwana | Free | Free |
| | Joint/Wanandoa | 3,000 | 3 |
| | Pensioners | Free | n/a |
| | Salary | 1,500 | 1 |
| | Bishop | Free | Free |
| | Priest/ Nun | Free | Free |
| | Wajasiriamali | 3,000 | n/a |
| | VIKOBA/ Informal Groups | Free | n/a |
| Cash Deposits | MKCB Accounts | Free | Free |
| | MKCB Agencies | Free | Free |
| | Bulk Cash | Free | Free |
| | Coins | Free | Free |
| | Small Denomination (1, 5, 10, and 20) | Free | Free |
| Over-the-counter withdrawal | **Current account** | | |
| | Business (SME, Corp., Sole-Propriators) | Below 5mln - 6,000 Above 5mln - 20mln - 8,000 Above 20mln - 0.12% max 100,000 | 0.1% min $/€/£ 2 max 50 |
| | Community (Parishes, Congregations, Schools, Hospitals, NGO's, Institutions) | Free | 1% on amount above $3,000 |
| | Call | Below 5mln - 5,000 Above 5mln - 20mln - 7,000 Above 20mln - 0.12% max 100,000 | n/a |
| | Personal/Individual | | 0.1% min $/€/£ 2 max 50 |
| | **Savings account** | | |
| | Business | Below 5mln - 5,000 Above 5mln - 20mln - 7,000 Above 20mln - 0.12% max | 0.1% min $/€/£ 2 max 50 |
| | Joint/Wanandoa | | |
| | Diocese/Parish/Jumuiya | Free | Free |
| | Personal | Below 5mln - 4,000 Above 5mln - 20mln - 6,000 Above 20mln - 0.12% max 100,000 | 0.1% min $/€/£ 2 max 50 |
| | Intergrity | 3,000 | 1 |
| | Student | Free | n/a |
| | Mwana | Above 5mln - 20mln - 5,000 Above 20mln - 0.12% max 100,000 | Free |
| | Salary | | 1 |
| | Wajasiriamali | | n/a |
| | Pensioners | Free | n/a |
| | Bishop | 3,000 | 1 |
| | Priest/ Nun | 3,000 | 1 |
| | VIKOBA/ Informal Groups | Free | n/a |

| Type of Charge | Item/Transaction | TZS | USD/EUR/GBP |
|---|---|---|---|
| Balance Enquiry | **Balance enquiry within banking hall** | | |
| | Call, Student | Free | n/a |
| | All other accounts | 1,000 | Free |
| | MKCB and Umoja Switch ATMs | 300 | n/a |
| | NMB ATM Balance enquiry | 500 | n/a |
| | MKCB mobile | 300 | n/a |
| | Balance enqiry - POS | 500 | n/a |
| | MKCB Internet Banking | Free | Free |
| | MKCB Mobile App | Free | Free |
| Account Statement | Umoja ATM Min statement | 500 | n/a |
| | NMB ATM Mini statement | 500 | n/a |
| | Mini statements - Agency Banking/POS | 500 | n/a |
| | Mobile Mini Statement | 500 | n/a |
| | E-Statement per month | Free | Free |
| | Adhock account statement on Banking Hall | 1,500 per page | 1.5 |
| Transaction Below Minimum Operating Balance | **Current account** | | |
| | Business (SME, Corp., Sole-Propriators) | 3,000 | 2 |
| | Community (Schools, Hospitals, NGO's, Institutions) | n/a | n/a |
| | Call | n/a | n/a |
| | Personal/Individual | 2,000 | 1 |
| | **Savings account** | | |
| | Business | 1,500 | 1.2 |
| | Diocese/Parish/Jumuiya | n/a | n/a |
| | Personal | 600 | 1.2 |
| | Intergrity | n/a | n/a |
| | Student | n/a | n/a |
| | Mwana | n/a | n/a |
| | Joint/Wanandoa | 600 | 1.2 |
| | Pensioners | n/a | n/a |
| | Salary | n/a | n/a |
| | Bishop | n/a | n/a |
| | Priest/ Nun | n/a | n/a |
| | Wajasiriamali | 500 | n/a |
| | VIKOBA/ Informal Groups | 500 | n/a |
| MKCB CDS Account | Treasury bills | 50,000 | n/a |
| | Treasury bonds | 100,000 | n/a |
| ATM and ID Cards Charges | Customer ID | Free | n/a |
| | Card Issuance (New) | 12,500 | n/a |
| | Card Replacement | 12,500 | n/a |
| | ATM monthly card maintainance | 500 | n/a |
| ATM Card Withdraw charge per transaction | **Umoja ATMs** | | |
| | Up to 49,999 | 1,500 | n/a |
| | Above 49,999 - 400,000 | 1,700 | n/a |
| | Failed transaction due to insufficient balance | 900 | n/a |
| | **NMB ATMs** | | |
| | Up to 99,999 | 2,000 | n/a |
| | Above 100,000 - 400,000 | 2,200 | n/a |
| | Failed transaction due to insufficient balance | 900 | n/a |
| Cash withdraw at MKCB Agency Banking | 1,000 - 50,000 | 1,000 | n/a |
| | 50,001 - 150,000 | 1,500 | n/a |
| | 150,001 - 200,000 | 2,000 | n/a |
| | 200,001 - 300,000 | 2,500 | n/a |
| | 300,001 - 400,000 | 3,000 | n/a |
| | 400,001 - 500,000 | 3,500 | n/a |
| | 500,001 - 600,000 | 4,000 | n/a |
| | 600,001 - 700,000 | 4,500 | n/a |
| | 700,001 - 800,000 | 5,000 | n/a |
| | 800,001 - 1,000,000 | 5,500 | n/a |
| | 1,000,001 - 1,500,000 | 6,000 | n/a |
| | 1,500,001 - 2,000,000 | 6,500 | n/a |
| | 2,000,001 - 2,500,000 | 7,000 | n/a |
| | 2,500,001 - 3,000,000 | 7,500 | n/a |
| | 3,000,001 - 7,000,000 | 8,000 | n/a |
| Cheque Deposit | Cheque from other Banks | Free | Free |
| | Inward Clearing | Free | Free |
| | Unpaid Cheque - (Refer to drawer) | 75,000 | Equiv. to TZS |
| Cheque Books | Cheque book costs per leaf (other current account) | 1,000 | 0.25 |
| | Cheque book costs per leaf (Community current account) | Free | Free |
| | Stop payment order per leaf | 30,000 | 15 |
| | Counter cheque per leaf | 10,000 | 10 |
| Bankers' Cheque | Commission per issued Bankers' Cheque | 30,000 | 15 |
| | Cancellation of Banker's cheque | 30,000 | 15 |
| Money Transfer MKCB to MKCB on USSD, MKCB App | Same currency | 1,000 | Equiv. to TZS |
| | Cross currency | | |
| Money Transfer (Within MKCB) | MKCB Agency Banking/POS | 1,500 | n/a |
| | Internal fund transfer - Backoffice | 1,500 | Equiv. to TZS |
| MKCB Internet/ Electronic Banking | Monthly fee per Retail user | Free | Free |
| | Monthly fee per Corporate user | Free | Free |
| | Cheque book request per leaf | n/a | n/a |
| | Internal fund transfer | 500 | Equiv. to TZS |
| | Multiple fund transfer per entry | 500 | Equiv. to TZS |
| | **Domestic Fund Transfer - EFT/TIPS:** | | |
| | Up to 50,000 | 500 | n/a |
| | 50,001 - 500,000 | 1,000 | n/a |
| | 500,001 - 5,000,000 | 1,500 | n/a |
| | 5,000,001 - 20,000,000 | 2,000 | n/a |
| | **Real Time Gross Settlement (TISS):** | | |
| | 1 - 10,000,000 | 2,000 | Equiv. to TZS |
| | 10,000,001 - 50,000,000 | 5,000 | Equiv. to TZS |
| | Above 50,000,000 | 8,000 | Equiv. to TZS |
| | Outgoing SWIFT Charge - Full Value Transfer | n/a | n/a |
| | Bulk Processing – Multiple Payment (Internal) | 500 | n/a |
| | **Bulk Processing – Multiple Payment (EFT)** | | |
| | Up to 50,000 | 500 | n/a |
| | 50,001 - 500,000 | 1,000 | n/a |
| | 500,001 - 5,000,000 | 1,500 | n/a |
| | 5,000,001 - 20,000,000 | 2,000 | n/a |
| | Bank to E-Wallet - Bulk Payment | As per the existing B2C charges | n/a |
| Bill Payments | Online bill payment services | Free | Free |
| GePG Payments | GePG Payments | n/a | n/a |
| Telegraphic Transfers (RTGS) | Incoming TISS and SWIFT | Free | Free |
| | **Outgoing Bank to Bank Transfer:** | | |
| | 1 - 10,000,000 | 2,000 | Equiv. to TZS |
| | 10,000,001 - 50,000,000 | 5,000 | Equiv. to TZS |
| | Above 50,000,000 | 10,000 | Equiv. to TZS |
| | Outgoing SWIFT Charge | Equiv. to USD | $ 60 |
| Standing Order Instructions | **Within MKCB: (On net)** | | |
| | Community Accounts | Free | Free |
| | Student Accounts | Free | Free |
| | Intergrity Accounts | Free | Free |
| | Call Accounts | n/a | n/a |
| | Other Accounts | 1,500 | 1 |
| | **To Other Banks:(Off net)** | | |
| | Call Accounts | n/a | n/a |
| | Other Accounts | 15,000 | n/a |
| | **Unpaid bankers orders due to inssufficient funds:** | | |
| | Call Accounts | n/a | n/a |
| | Student Accounts | n/a | n/a |
| | Other Accounts | 30,000 | 30,000 |

| Type of Charge | Item/Transaction | TZS | USD/EUR/GBP |
|---|---|---|---|
| Mobile Banking Charges | **Transfer from MKCB to MNOs: (B2C)** | | |
| | 0 - 50,000 | 1,000 | n/a |
| | 50,001 - 100,000 | 1,500 | n/a |
| | 100,001 - 300,000 | 2,000 | n/a |
| | 300,001 - 500,000 | 3,000 | n/a |
| | 500,001 - 1,000,000 | 4,000 | n/a |
| | 1,000,001 - 1,500,000 | 5,000 | n/a |
| | 1,500,001 - 3,000,000 | 6,000 | n/a |
| | Internal Bank Account Transfer | 500 | n/a |
| | Transfer from MNOs to Bank (C2B) | n/a | n/a |
| | Balance Enquiry | 300 | n/a |
| | Mini statement | 500 | n/a |
| Electronic Fund Transfer (EFT) | Incoming to MKCB Bank | Free | Free |
| | **Ongoing or Outward to other Bank** | | |
| | Up to 50,000 | 500 | n/a |
| | 50,001 - 500,000 | 1,000 | n/a |
| | 500,001 - 5,000,000 | 1,500 | n/a |
| | 5,000,001 - 20,000,000 | 2,000 | n/a |
| General Account Operation and MKCB POS issuance fee for Agency Banking | Certificate of balances | 30,000 | Equiv. in TZS |
| | Confirmation to auditors | 30,000 | Equiv. in TZS |
| | Search for information less than 1 year | n/a | n/a |
| | Search for information over 1 year but not exceeding 5 years | n/a | n/a |
| | Search for information over 5 years | 30,000 | Equiv. in TZS |
| | Status Report upon customers' request | 30,000 | Equiv. in TZS |
| | Salary processing manual transaction per entry | 500 | Equiv. in TZS |
| | Salary processing and bulk 'payment within MKCB | 500 | Equiv. in TZS |
| | Salary processing and bulk 'payment outside MKCB | n/a | n/a |
| | Dormant account activation | Free | Free |
| | Closing account less than six month old (except SGL) | 30,000 | 15 |
| | Monthly charge drawn below minimum balance | 10,000 | $2/EUR2.5/GBP1.5 |
| | Mkombozi WAKALA outlet application fee | 300,000 | n/a |
| Delibarate closing of accounts | Business Current | 20,000 | 20 |
| | Personal Current | 10,000 | 10 |
| | Personal Savings | 5,000 | 5 |
| | Wajasiriamali | 2,000 | n/a |
| | Joint Accounts | 5,000 | 5 |
| | Other MKCB Accounts | Free | Free |
| Cash Change | Cash coin per bag of TZS 100,000 | Free | n/a |
| Dormant Accounts activation fee | All accounts | Free | Free |
| ATM Withdrawal Limit Per Day | Umoja Card Via Umoja Switch ATMs | 3,000,000 | n/a |
| | Umoja Card Via NMB ATMs | 3,000,000 | n/a |
| MKCB Mobile Transfer Per Day | Within MKCB (Account to account) | n/a | n/a |
| | Outside MKCB ( To other Bank) | 20,000,000 | n/a |
| | Outside MKCB (To MNO's - Tigo Pesa, M-Pesa, Airtel Monet etc) | 10,000,000 | n/a |
| | Bill payments | 1,000,000 | n/a |
| Other Limits | LUKU Purchase on MKCB mobile (per day) | 1,000,000 | n/a |
| | MKCB Agency Banking (max. per transaction) | 7,000,000 | n/a |
| | MKCB Agency Banking - Cardless Cash Withdrawal (max. per transaction) | 7,000,000 | n/a |
| | Airtime purchase daily limits | 1,000,000 | n/a |
| CIT Services | Per trip | 101,755 | Equiv to TZS |
| Letter of Credit | **Imports LC's** | | |
| | Opening LC | Equivalent to FCY | 1% pq min 250 |
| | Confirmation | Equivalent to FCY | 1% pq min 250 |
| | Ammendments | Equivalent to FCY | 120 flat fee |
| | Swift Charges | Equivalent to FCY | 60 |
| | LC acceptance | Equivalent to FCY | 0.1% |
| | Extension (Tenor and or, amount) | Equivalent to FCY | 1% pq min 250 |
| | Cancellation | Equivalent to FCY | 200 |
| | **Exports LC's** | | |
| | Payment chaser | Equivalent to FCY | 50 |
| | Advising Commission - Customer | Equivalent to FCY | % min 200 max 350 |
| | Advising Commission - To other Banks | Equivalent to FCY | 350 |
| | Confirmation charge | Equivalent to FCY | 1.2% min 300 pq |
| | Documents verification | Equivalent to FCY | 150 |
| | Negotiation Charge | Equivalent to FCY | 0.6% min 200 |
| | Discripancy fee | Equivalent to FCY | 120 |
| | Postage | Equivalent to FCY | 30 |
| | Courier charges | Equivalent to FCY | 70 |
| | Ammendments | Equivalent to FCY | 120 flat fee |

| Type of Charge | Item/Transaction | TZS | USD/EUR/GBP |
|---|---|---|---|
| Bonds and Guarantees | **Bid Bonds:** | | |
| | Unsecured | 3% pq or part there of; | Eqivalent to TZS |
| | Cash Cover | 0.6% pq or part there of; | Eqivalent to TZS |
| | Secured by other collaterals | 2% pq or part there of; | Eqivalent to TZS |
| | **Guarantees:** | | |
| | Advance Payment, Perfomance Bond and others | | |
| | Cash Cover | 0.6% pq or part there of; | Eqivalent to TZS |
| | Secured by other collaterals | 2% pq or part there of; | Eqivalent to TZS |
| TIME Deposit | 3 months | 3% p.a | 0.305% p.a |
| | 6 months | 4% p.a | 0.65% p.a |
| | 9 months | 5% p.a | 1.10% p.a |
| | 12 months | 6% p.a | 1.15% p.a |
| | 18 months | 7% p.a | 1.35% p.a |
| | 24 months | 8% p.a | Negotiable |
| | 36 months | 9% p.a | |
| | Amount above TZS 100 Million | Negotiable | |
| Loans and Advance | **Business Loans** | | |
| | Interest Rate (Per annum & Reducing) | 17% - 25% | 9% - 11% |
| | Application fee | 100,000 | 100 |
| | Commitment fee | 1.2% | 1% |
| | Management fee | 2.5% | 1% |
| | Key Man Insurance (Sole Propriator) | 0.7% | 0.7% |
| | Security discharge fee | 80,000 | Equiv. to TZS |
| | Penalty on late payment - Per annum | 38% | Equiv. to TZS |
| | Early settlement fee | 5% | n/a |
| | **Agriculture Loans** | | |
| | Interest Rate (Per annum & Reducing) | 17% - 25% | 9% - 11% |
| | Application fee | 100,000 | 100 |
| | Commitment fee | 1.2% | 1% |
| | Management fee | 2.5% | 1% |
| | Key Man Insurance (Sole Propriator) | 0.7% | Equiv. to TZS |
| | Security discharge fee | 80,000 | Equiv. to TZS |
| | Penalty on late payment - Per annum | 26% | Equiv. to TZS |
| | Early settlement fee | 5% | n/a |
| | **Housing Micro Finance Loans** | | |
| | Interest Rate (Per annum & Reducing) | 29.0% | n/a |
| | Application fee | 100,000 | n/a |
| | Commitment fee | 1.2% | n/a |
| | Management fee | 2.5% | n/a |
| | Key Man Insurance (Sole Propriator) | 0.7% | n/a |
| | Security discharge fee | 80,000 | n/a |
| | Penalty on late payment - Per annum | 27.0% | n/a |
| | Early settlement fee | 5% | n/a |
| | **Insurance Premium Financing** | | |
| | Interest Rate (Per annum & Reducing) | 15% | 7% - 9% |
| | Penalty on late payment - Per annum | 15% | Equiv. to TZS |
| | **Mortgage Loans** | | |
| | Interest Rate (Per annum & Reducing) | 18.0% | n/a |
| | Application fee | 100,000 | n/a |
| | Commitment fee | 1.2% | n/a |
| | Management fee | 2.5% | n/a |
| | Security discharge fee | 80,000 | n/a |
| | Penalty on late payment - Per annum | 27.0% | n/a |
| | Early settlement fee | 5% | n/a |
| | **Salaried Loans** | | |
| | Interest Rate (Per annum & Reducing) | 18% | n/a |
| | Commitment fee | 2.5% | n/a |
| | Credit life insurance | Private Sector - 1.2% Public Sector - 2% | n/a |
| | Security discharge fee | 80,000 | n/a |
| | Early settlement fee | 5% | n/a |
| | **SGL** | | |
| | Interest Rate (Per month) | 4.3% | n/a |
| | Membership registration fees | 2,500 | n/a |
| | Commitment fee | 2.5% | n/a |
| | Penalty on late payment - Per annum | 5.1% | n/a |
| | **Pensioners Loan** | | |
| | Interest Rate (Per annum & Reducing) | 18% | n/a |
| | Commitment fee | 1% | n/a |
| | Credit life insurance | 2% | n/a |
| | Early settlement fee | 5% | n/a |

**Disclaimer:**

* These costs are exclusive of Value Added Tax (VAT) & Government chargess.
* In an event that a customer has a limited balance amount to cover the fee, the Bank has a right to deduct partial amount of the respective fee/charge and the balance upon amount availability.
* Loan Interest rates are indicative, actual pricing shall depend on the type and risk level of the underying client and business.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua Madhubuti zichukuliwe kumaliza machafuko DR Congo

**HALI** si shwari katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kutokana na machafuko yanayoendelea nchini humo. Chanzo cha machafuko hayo ni waasi wa M23 wanaodaiwa kuungwa mkono na Rwanda kuendelea kusonga mbele kwa takriban siku nne mfululizo,

Taarifa zilizoripotiwa juzi zilibainisha kwanba takriban watu 100 wameuawa katika mji wa Goma ulioko jimbo la Kivu ya kaskazini. Taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vya Habari pia zilibainisha kuwa zaidi ya watu 1,000 walijeruhiwa hadi juzi huku makazi ya watu yakiharibiwa pamoja na kusababisha ukosefu wa huduma muhimu za kijamii kama maji, umeme na chakula.

Wakati hayo yakiendelea, wananchi katika jiji la Kinshasa juzi waliandamana barabarani na kuchoma magurudumu huku wakishambulia ofisi za ubalozi za Rwanda, Ufaransa, Marekani, Ubelgiji, Afrika Kusini, Kenya na Uganda. Afrika Kusini pia imesema wanajeshi wake wanne walioko huku kwenye majeshi ya kulinda amani wameuawa.

Baadhi ya mataifa yameelekeza shutuma kwa Rwanda kuwa inawafadhili wapiganaji hao wa M23 kwa madai kwamba wanafanya hivyo kwa ajili ya kuiba rasilimali za DRC kama vile madini na vito ambazo zinapatikana kwa wingi nchini humo. Hata hivyo, Rais Paul Kagame wa Rwanda amekanusha na kusema wapiganaji hao si raia wa Rwanda bali ni wahamiaji wanaojificha nchini humo na kufanya uhalifu Congo.

Jambo ambalo linaonesha kuchochea zaidi tatizo hilo ni kauli ya viongozi wa serikali ya DRC kuwataka vijana kubeba silaha na Kwenda mstari wa mbele kupambana na wapiganaji hao iliyowaita kuwa wavamizi.

Hofu pia imezidi kutanda huku mataifa mbalimbali ikiwamo Marekani yakitaka raia wao walioko DRC waondoke mara moja kuepuka maafa yanayoweza kuwapata kutokana na mashambulizi hayo. Wakati Marekani ikiwataka raia wake waondoke, Umoja wa Ulaya (EU) umesema vitendo hivyo havikubaliki na vinazua wasiwasi mkubwa.

Kuna juhudi mbalimbali zinazochukuliwa ili kusitisha mapigano hayo na viongozi wa mataifa mbalimbali na jumuiya za kikanda zimeonesha nia thabiti ya kumaliza tatizo hilo. Rais Samia Suluhu Hassan, kwa mfano, juzi aliitisha kikao cha viongozi wakuu wa nchi za Jumuiya ya maendeleo Kusini mwa Afrika kwa ajili ya kutafuta namna ya kufikiwa mwisho kwa machafuko hayo.

Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini na mwenzake wa Rwanda, Paul Kagame, nao wamekubaliana kuhusu hitaji la dharura la kusitishwa kwa mapigano hayo na kuanzishwa kwa mazungumzo ya amani baina ya pande zinazohusika.

Utashi wa viongozi hao ni hatua kubwa katikak kuhakikisha amani ya kudumu inapatikana ndani ya eneo hilo, nchi za Maziwa Makuu na ukanda wa Afrika Mashariki na kusini mwa Afrika kwa ujumla. Kwa mantiki hiyo, mpango wa kutaka kusitishwa kwa mapigano hayo, ni hatua ya kupongezwa kwa kuwa imeonesha mpango chanya katika kumaliza tatizo.

Licha ya jitihada hizo, ni wakati mwafaka pia SADC na Umoja wa Afrika (AU) kuchukua hatua zaidi katika kukomesha mapigano hayo. Si mara ya kwanza kwa jumuiya hizo kuchukua hatua dhidi ya waasi hao ambao wanasababisha uvunjifu wa amani na kugharimu maisha ya watu wasio na hatia. Tanzania pia iliwahi kushiriki operesheni ambayo iliwasambaratisha waasi hao na kutokomea walikotoka na kuacha ardhi ya DRC katika hali ya usalama.

Ni wakati mwafaka hatua za kila aina kuchukuliwa ili kuilinda Congo na rasilimali zake ambazo miaka nenda rudi zimekuwa zikichukuliwa na kunufaisha watu wengine kwa kutumia kivuli cha waasi. DRC yenye amani inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Frank Monyo

## Muungwana Lazima Nilonge

# Itapendeza zaidi msaada kwa watoto njiti iwe kisera, sheria

**MTOTO** katika namna ni zawadi ya jamii, mbali na makao makuu yake, kwa wazazi baba, mama au walezi wakuu.

Tafsiri hiyo inapanuka kwa mustakabali wa familia anapozaliwa mtoto huyo, wao hujisikia tabasamu kubwa na wanapenda awe na yote mazuri, hivyo anapopatwa na kasoro za kibinadamu, wana familia na jamii hujisikia huzuni. Hilo ndilo linafika akiwa mtoto njiti.

Hali inakuwa ngumu kwa familia, kwani wazazi hukutana na changamoto kubwa kwenye malezi, pia katika mazingira ya kazi, katika taasisi za umma na binafsi, kutokana na sera za kazi mara nyingi hazilengi mahitaji maalum ya wazazi hao.

Katika sehemu nyingi za kazi na hasa kuajiriwa, kuna walakini wa mazingira ya kutozingatiwa kuwajali wazazi wa watoto njiti na mustakabali wa malezi yao hapo waliko.

Niseme, hizi hapa ni baadhi tu ya changamoto wanazozikabili ikiwamo ukosefu wa maeneo maalum kwa ajili ya kunyonyesha, kupumzika, au kutoa maziwa ya akiba.

Ni wazi kwamba wazazi wanahitaji muda wa ziada wa kuwahudumia watoto wao njiti na mara nyingi, hukutana na vikwazo, kwani taasisi nyingi hazina maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli hizi.

Nchini kwetu, hata mwaka jana katika kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani, mnamo Mei Mosi, Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, akalielekeza kuwa mfanyakazi atakayejifungua mtoto njiti, kipindi cha uangalizi maalum hakiwezi kuhesabiwa kama likizo ya uzazi.

Akasisitiza kwamba hesabu ya likizo kutoka kwa mwajiri itaanza, baada ya mtoto kumaliza kipindi cha uangalizi maalum, kulingana na tathmini ya madaktari.

Ni jambo lililoibua furaha kwa wafanyakazi walioshiriki tukio hilo, Dk. Mpango akiendelea kusema kuwa mfanyakazi ataruhusiwa kutoka kazini kwa muda wa miezi sita baada ya likizo ya uzazi, ili kumwezesha kwenda kunyonyesha mtoto wake.

Dk. Mpango akasisitiza suala la afya ya mama na mtoto, hususan aliye njiti ni kipaumbele kikubwa kwa serikali ya awamu ya sita.

Kauli hii ya mpango inayoakisi aliyoyafanya Rais Samia Suluhu Hassan, kutuma salamu za pongezi na zawadi ya fedha taslimu kiasi cha shilingi milioni mbili kwa Mariam Mwakabungu (25) anayejitolea kukumbatia watoto njiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Amana, jijini Dar es Salaam.

Hapo binafsi, narusha kongole kwa serikali kujali afya ya mama na mtoto katika picha hiyo pana.

Uhalisia ni kwamba, watoto hawa waliozaliwa kabla ya muda wa kutoka tumboni kwa mama, wanahitaji uangalizi wa karibu, wana mahitaji maalum, pia muda wa ziada wa mzazi, pasipo kusahau upendo wa ziada.

Hayo yote hayatakuwa na maana, endapo waajiri kazini hawatazingatia maagizo hayo na hatua za serikali wakiweka mazingira rafiki kwa wafanyakazi wao wanaojifungua watoto njiti.

Ni wakati sasa wa taasisi za umma na binafsi kuweka utaratibu rafiki kwa kuboresha sera na miongozi itakayowaongoza wafanyakazi ambao watajifungua watoto njiti.

Na hili sio kwamba ni la kwetu peke yetu nchini, la hasha! Ukidodosa nguzo za kimataifa, kuna taasisi za Umoja wa Mataifa; Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Kazi Duniani (ILO), tayari kimataifa zimeshatoa miongozo kwa miaka sasa, zinazolenga kulinda afya ya mama na mtoto, pamoja na haki za wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti.

Hapo zinagusa huduma bora kwa mama na mtoto, ikiwa ni pamoja na uangalizi maalum kwa viumbe hao.

Naiona hiyo kuwa ngazi kwetu kiserikali inatusukuma kufanya mapitio tukawa na sera, pia sheria ua vipengele katika ajira, iwe na miongozo ya namna ya kumsaidia mzazi mwenye mtoto njiti.

Najua kuna mambo kadhaa ya kiserikali na asasi binafsi yenye msaada wa moja kwa moja kwao wazazi, walezi na wahusika walio njiti.

Pale inapokuwa katika sura ya kisera na kisheria, inaidhinisha kuwapo mwongozo wa lazima ambao mambo haya kuwa utararibu

## TANGAZO

# UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 31/12/2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo mwaka ya 31.12.2024 | Robo mwaka ya 30.09.2024 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| 1 | Fedha tasilimu | 1,802 | 1,799 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 4,801 | 3,886 |
| 3 | Uwekezaji katika amana serekalini | 3,919 | 2,766 |
| 4 | Salio katika benki nyingine na taasisi za fedha | 7,390 | 6,874 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushuhulikiwa | 97 | 96 |
| 6 | Miamala baina ya matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili zililizo afikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za wateja zilizo kubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | 2,368 | 1,004 |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 43,303 | 41,009 |
| 12 | Mali nyingine | 2,857 | 2,323 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | 35 | 35 |
| 14 | Akauti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali zisizohamishika , mitambo na vifaa | 2,421 | 2,459 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **68,993** | **62,251** |
| | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na taasisi za fedha | 0 | 0 |
| 18 | Amana za wateja | 47,531 | 45,170 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha tasilimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya malipo/fedha za kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na hawala za kibenki zilizotolewa | 0 | 0 |
| 23 | Limbiko za kodi na gharama zitakazolipwa | 247 | 330 |
| 24 | Dhima la tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala isiyoshuhulikiwa baina ya matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazolipwa baadae | 0 | 0 |
| 27 | Dhima nyingine | 527 | 628 |
| 28 | Madeni | 4,000 | 0 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **52,305** | **46,128** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 29)** | **16,688** | **16,123** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 14,348 | 14,039 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | -64 | 37 |
| 34 | Faida (hasara) ya kipindi husika | 1,152 | 795 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 1,252 | 1,252 |
| 36 | Stahiki ya mwenye hisa chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **16,688** | **16,123** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | 5,407 | 5,988 |
| 39 | Mikopo chechefu | 2,685 | 2,564 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 1,042 | 961 |
| 41 | Malinyingine chechefu | 0 | 0 |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 24.19% | 25.90% |
| | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 5.90% | 5.97% |
| | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 86.05% | 92.92% |
| | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 62.76% | 65.88% |
| | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 79.16% | 81.36% |
| | Ongezeko la amana | 5.23% | 5.25% |
| | Ongezeko la mali | 10.83% | 5.29% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO YA MWAKA UNAOISHIA 31/12/2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka wa sasa 31.12.2024 | Robo ya Mwaka Linganishi 31.12.2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31.12.2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Mapato ya riba** | **2,129** | **1,655** | **7,665** | **6,598** |
| 2 | Gharama za riba | 435 | 467 | 1,942 | 1,702 |
| 3 | Madeni viza yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 4 | **Mapato halisi ya riba (1 kutoa 2)** | **1,613** | **1,148** | **5,470** | **4,738** |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | 81 | 40 | 253 | 158 |
| 6 | **Mapato yasiyo na riba** | **375** | **340** | **1384** | **1350** |
| | 6.1 Faida /hasara zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | -23 | 37 | 76 | 106 |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 394 | 267 | 1280 | 1127 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato mengine | 4 | 36 | 28 | 117 |
| 7 | **Gharama zisizo za riba** | **1,614** | **1,429** | **5,693** | **5,007** |
| | 7.1 Mishahara na mafao | 830 | 720 | 2,901 | 2457 |
| | 7.2 Ada na kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama nyingine za uendeshaji | 784 | 709 | 2,792 | 2550 |
| 8 | **Faida/(hasara) ya uendeshaji** | **374** | **59** | **1,161** | **1,081** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | 72.5 | -66 | 290 | 216 |
| 10 | **Faida/(hasara) halisi baada ya kodi ya mapato** | **302** | **125** | **871** | **865** |
| 11 | Mapato mengine yaliojumuishwa (bainisha) | 4 | 50 | 281 | 260 |
| 12 | **Jumla ya faida /(hasara) iliojumuishwa kwa mwaka** | **306** | **175** | **1,152** | **1,125** |
| 13 | idadi ya waajiriwa | 54 | 51 | 54 | 51 |
| 14 | mapato kwa hisa | 2.13% | 1.37% | 8.03% | 8.80% |
| 15 | idadi ya matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | **BAHADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | uwiano wa faida kabla ya kodi na watani wa mali | 0.47% | 0.23% | 1.76% | 2.10% |
| | uwiano wa faida kabla ya kodi na watani wa fedha za wanahisa | 1.86% | 0.89% | 7.02% | 7.97% |
| | uwiano wa matumizi yasiyo ya riba na mapato ghafi | 64.46% | 71.63% | 62.91% | 63.00% |
| | uwiano wa mapato halisi ya riba na wastani ya mali zinazozalishwa | 3.83% | 3.18% | 12.02% | 13.13% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31/12/2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za uendeshaji** | Robo ya mwaka ya sasa 31.12.2024 | Robo ya Mwaka 30.09.2024 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31.12.2024 | Limbikizo la mwaka Linganishi 31.12.2023 |
|---|---|---|---|---|
| **Mapato/(hasara) halisi** | **378** | **435** | **1,442** | **1,341** |
| **Marekebisho kwa ajili ya:-** | - | - | - | - |
| Uchakavu | 140 | 118 | 568 | 392 |
| **Badiliko halisi katika mikopo** | **(2,294)** | **(3,238)** | **(6,314)** | **(4,528)** |
| Faida / (hasara) kwenye mauzo ya mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika amana | 1,861 | 2,254 | 7,065 | 4,164 |
| Mabadiliko katika amana za muda mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko katika dhamana ya Hazina | (1,153) | 575 | (3,919) | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (184) | (64) | (146) | 728 |
| Mabadiliko halisi katika mali nyingine | (534) | 170 | (262) | (900) |
| Kodi iliyopitwa | (73) | (72) | (290) | (216) |
| Mengineyo (bainisha) | 370 | (104) | (1,199) | (246) |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za uendeshaji** | **(1,489)** | **74** | **(3,055)** | **735** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za uwekezaji** | | | | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa mali za kudumu | (21) | (165) | (220) | (110) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa amana zisizoshuhulikiwa mawakala | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshuhulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za uwekezaji** | **(21)** | **(165)** | **(220)** | **(110)** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za kifedha** | | | | |
| Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | - |
| Ongezeko la hisa | 309 | 618 | 1,565 | 2,574 |
| Gawio lililolipwa kwa fedha taslimu | - | - | - | (821) |
| Mabadiliko halisi katika madeni mengine | 4,000 | - | 3,722 | (555) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za kifedha** | **4,309** | **618** | **5,287** | **1,198** |
| **Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko /punguzo katika fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | **2,800** | **527** | **2,012** | **1,823** |
| Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/mwaka | 13,659 | 13,132 | 14,446 | 12,623 |
| **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/mwaka** | **16,458** | **13,659** | **16,458** | **14,446** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO YA MWAKA ULIOISHIA 31.12 . 2024

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| **Mr. Samwel A. Wado (Ofisa Mtendaji Mkuu)** | **S. Wado** | **31 Januari, 2025** |
| **Mrs. Anita Joseph Mnkeni ( Mkuu wa Idara ya Fedha)** | **A.MNKENI** | **31 Januari, 2025** |
| **Mr. Emmanuel Kessy (Mkuu wa Idara ya Ukaguzi )** | **E.Kessy** | **31 Januari, 2025** |

**Usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| **1. Dr. Heavenlight Kavishe (Mwenyekiti wa Bodi)** | **H.Kavishe** | **31 Januari, 2025** |
| **2.Mr. Munguatosha M. Makyao (Mkurugenzi)** | **M.Makyao** | **31 Januari, 2025** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31/12/2024

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya kwanza inayoanza 01.01.2024** | **12,783** | **17** | **58** | **1,169** | **30** | **36** | **14,093** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato 31.12.2024 | 0 | 0 | 1152 | 0 | 0 | 0 | **1,152** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 1,565 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1,565** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mabadiliko katika tengo la mikopo chechefu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | -122 | 0 | 0 | 0 | **-122** |
| **Salio la mwisho wa robo ya tatu ya mwaka 31.12.2024** | **14,348** | **17** | **1,088** | **1,169** | **30** | **36** | **16,688** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2023** | **10,209** | **17** | **1,017** | **596** | **30** | **68** | **11,937** |
| Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 2,574 | - | - | - | - | - | 2,574 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa(Gawio lililolipwa ) | - | - | (821) | - | - | - | (821) |
| Kodi iliyopita na mikopo iliyofutwa | - | - | (848) | - | - | - | (848) |
| Ziada Juu ya Hisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (573) | 573 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Kupungua kwa ruzuku za Mtaji | - | - | - | - | - | (32) | (32) |
| Hamisho kutoka faida au Hasara | - | - | 1,283 | - | - | - | 1,283 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2023** | **12,783** | **17** | **58** | **1,169** | **30** | **36** | **14,093** |


## UCB OFFERS THE FOLLOWING PRODUCTS:

- *Savings Accounts*
- *Current Account*
- *Elimu Juniour Account*
- *Mavuno Savings Account*
- *Uchumi Savings Account*
- *Fixed Deposit Accounts-(FDR) with attractive Rates*
- *Forex Accounts*
- *Bureau De Change*
- *ATMs Services,all over the Country-Umoja Switch*

CARING FOR FAMILY ECONOMY



Uzalishaji umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania kuuza umeme nje: Uhalisia, fursa na manufaa ya kiuchumi



**Na Khaled Gwiji**
**Simu: +1 437 431 6747**
**Barua pepe: khaleed_ihaab@yahoo.com**

TANGAZO la Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kwamba nchi iko tayari kuuza na kusambaza umeme kwa mataifa jirani limeibua mjadala mpana. Wakosoaji wanahoji kama je, ni busara kuuza umeme nje wakati bado kuna changamoto za usambazaji nishati hiyo ndani ya nchi?

Hata hivyo, uchambuzi wa kina unaonyesha kuwa kuuza umeme nje si ishara ya uhaba wa nishati, bali ni hatua ya kimkakati inayoweza kuimarisha uchumi wa taifa; kwani biashara ya nishati, kama zilivyo biashara nyingine, haifanywi kwa mtazamo wa kujitosheleza kwanza bali kwa misingi ya fursa za kiuchumi na ushirikiano wa kikanda. Hivyo, biashara ya umeme inategemea ziada ya uzalishaji, mahitaji ya soko na fursa za kiuchumi.

**UZALISHAJI NA MAHITAJI YA UMEME TANZANIA**

Kwa sasa, Tanzania inazalisha takriban megawati 3,600, huku mahitaji ya ndani yakiwa megawati 1,800. Hii ina maana kuwa kuna ziada ya takriban megawati 1,800, kiasi ambacho kinaweza kuuzwa kwa mataifa jirani kama Kenya, Zambia, Malawi, na kadhalika.

Changamoto kubwa inayokabili sekta ya nishati nchini si uhaba wa umeme, bali ni upanuzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji, hasa katika maeneo ya vijijini. Kwa mujibu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kiwango cha upatikanaji wa umeme nchini kimefikia asilimia 75, lakini bado kuna maeneo yanayohitaji uwekezaji zaidi ili kufikiwa. Katika mazingira haya, kuuza umeme nje si tu kwamba ni jambo linalowezekana, bali pia ni fursa ya kiuchumi inayoweza kusaidia kuboresha sekta ya nishati nchini.

**JE, LAZIMA NCHI IJITOSHELEZE KABISA KABLA YA KUUZA?**

Hoja ya kwamba nchi lazima ijitosheleze kikamilifu kabla ya kuuza bidhaa au huduma nje si sahihi katika uchumi wa kisasa. Katika uchumi wa soko huria, si lazima nchi ijitosheleze kikamilifu kwa bidhaa fulani ndipo ianze kuiuza nje. Badala yake, biashara hasa ya kimataifa huendeshwa kwa misingi ya fursa, mahitaji ya soko, na faida za kiuchumi. Mifano halisi kutoka mataifa mengine inaonyesha kuwa:

- Nigeria inauza mafuta ghafi nje ya nchi licha ya kuwa na changamoto za kusambaza bidhaa za petroli kwa wananchi wake.
- Kenya inauza chai ya hadhi ya juu kwenye soko la kimataifa, huku baadhi ya wananchi wake wakishindwa kumudu bei ya chai hiyo ndani ya nchi.
- Ethiopia inauza umeme kwa Kenya na Sudan, ingawa bado kuna changamoto za usambazaji wa umeme katika maeneo yake ya ndani.

Hii inaonyesha kuwa kuuza umeme nje haikumaanishi kwamba mahitaji ya ndani hayajazingatiwa. Badala yake, ni mkakati adhimu na mahsusi wa kuongeza mapato na kuvutia uwekezaji zaidi katika sekta ya nishati.

**CHANGAMOTO YA SGR: UHALISIA NA UKWELI HALISI**

Baadhi ya wakosoaji wanadai kuwa tukio la reli ya kisasa (SGR) kusimama maporini ni dalili ya uhaba wa umeme nchini. Hata hivyo, serikali imeeleza kuwa tukio hilo lilitokana na hitilafu za kimitambo na si kwa sababu ya ukosefu wa umeme.

Sambamba, Teknolojia yoyote ya kisasa inaweza kukumbwa na changamoto za kiufundi, lakini hilo halihusiani moja kwa moja na upatikanaji wa umeme nchini. Kutumia tukio hili kama hoja ya kupinga uuzaji wa umeme nje ni tafsiri isiyo sahihi ya hali halisi ya sekta ya nishati Tanzania.

**FAIDA ZA KUUZA UMEME NJE YA NCHI**

**1. Mapato ya Kigeni**

Tanzania inaweza kuingiza mapato ya kigeni kwa kuuza umeme kwa mataifa jirani. Mataifa kama Ethiopia na Msumbiji tayari yanatumia fursa hii:

- Ethiopia inapata mabilioni ya dola kwa kuuza umeme kwa Kenya, Sudan, na Djibouti, fedha ambazo zimeiwezesha kuwekeza katika miradi mikubwa ya nishati kama Bwawa la Grand Ethiopian Renaissance (GERD).
- Msumbiji inauza umeme kwa Afrika Kusini kupitia Mradi wa Cahora Bassa, na mapato hayo yametumika kuboresha miundombinu ya nishati nchini humo.

Tanzania inaweza kutumia mfano huu kuongeza mapato yatakayowezesha uboreshaji wa sekta ya nishati.

**2. Kuvutia Uwekezaji**

Uuzaji wa umeme nje unaweza kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika miradi mikubwa ya kuzalisha nishati. Fursa hii inaweza kusaidia katika:

- Ujenzi wa mitambo mipya ya kuzalisha umeme.
- Upanuzi wa mtandao wa usambazaji wa umeme kufikia maeneo ambayo bado hayajaunganishwa.

3. Kuboresha Miundombinu ya Usambazaji

Mapato yanayopatikana kutokana na kuuza umeme nje yanaweza kutumika katika:

- Kuboresha na kupanua miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini.
- Kuwezesha upatikanaji wa umeme vijijini na kupanua huduma kwa Watanzania wengi zaidi.

Miradi mikubwa ya nishati inayofanikisha uuzaji wa umeme.

Katika juhudi za kuongeza uzalishaji wa umeme, Tanzania inatekeleza miradi mikubwa, ikiwamo Bwawa la Nyerere, ambalo linatarajiwa kuzalisha megawati 2,115. Mradi huu utazalisha zaidi ya mara moja ya mahitaji ya sasa ya nchi, hivyo kutoa fursa ya kuuza umeme wa ziada.

Zaidi ya hapo, Tanzania imeshajiunga na mataifa jirani kupitia Mradi wa Rusumo, ambao utawezesha biashara ya umeme kati ya Tanzania, Kenya, Burundi, na Rwanda. Viongozi wa mataifa haya wanatarajiwa kuzindua rasmi mradi huo hivi karibuni, inshaa'Allah.

Kuuza umeme nje ya nchi si dalili ya uhaba wa nishati, bali ni mkakati wa kuimarisha uchumi wa Tanzania. Biashara ya umeme inaweza kusaidia kuongeza mapato ya kigeni, kuvutia uwekezaji, na kuimarisha usambazaji wa umeme kwa Watanzania.

Badala ya kuangalia changamoto kwa mtazamo wa upande mmoja pekee, ni muhimu pia kuelewa kwamba Tanzania ina nafasi ya kuwa kinara wa nishati katika Afrika Mashariki na Kusini. Kwa uwekezaji sahihi na mipango madhubuti, nchi inaweza kufaidika kwa kuuza umeme, huku ikiendelea kuboresha upatikanaji wa nishati kwa wananchi wake.

Serikali inapaswa kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya kusafirisha umeme, kushirikiana na mataifa jirani, na kuhakikisha kuwa uuzaji wa umeme unaleta manufaa kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

# Serikali yakaza amri kupeleka ndizi Z'bar

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imesisitiza kuwa amri ya kupiga marufuku usafirishaji ndizi na machipukizi ya migomba kwenda visiwa vya Zanzibar iko pale pale ili kudhibiti kusambaa Virusi vya Fungashada la Migomba (BBTV) Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa amri hiyo, mfanyabiashara wa Tanzania Bara au mchukuzi, haruhusiwi kusafirisha zao hilo la chakula na biashara kwenda visiwa vya Unguja na Pemba vya Zanzibar ili kunusuru kufa, hasara kwa wakulima na kunusuru pato la taifa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Afya ya Mimea wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), Dk. Ben Ngowi, alitoa amri hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo katika warsha inayoendelea mjini hapa Mkoa wa Kilimanjaro, kuandaa rasimu ya mkakati na mpango kazi wa kutokomeza ugonjwa huo.

"Kwa Tanzania Zanzibar, kumefanyika survey (tafiti) mbalimbali, hazijaonyesha kwamba ugonjwa huu wa fungashada la migomba umeingia Zanzibar; na Zanzibar ni walaji nwazuri wa ndizi kama ilivyo Tanzania Bara, lakini ni kutokana na umuhimu kwenye chakula cha Mzanzibar, na ndio maana mamlaka ya Zanzibar, imeona kuna haja ya kulinda hizi ndizi zetu.

"Sasa katika kufanya hilo Plant Protection Service ya Zanzibar, inafanya juhudi kuhakikisha ugonjwa huu hauendi kule. Mojawapo ya hatua ilizochukua ni kuhakikisha mfanyabiashara yeyote wa Tanzania Bara au mchukuzi yeyote wa ndizi aliye Tanzania Bara haruhusiwi kusafirisha kwenda Unguja na Pemba, machipukizi ya migomba," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Ngowi, machipukizi hayo ndio mbegu yenyewe, hivyo TPHPA wamepiga kambi bandari za Dar es Salaam, Tanga, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) na vituo vya mipakani kuhakikisha hilo halifanyiki.

"Hata kama ni ndizi za kawaida ambazo zina mashambulizi, ule mkungu wa ndizi haturuhusu uende Zanzibar, isije kuwa ni chanzo ikaenda ikaingiza ugonjwa huo Zanzibar,"alisema Mkurugenzi huyo wa Usalama wa Afya ya Mimea.

Mtaalamu wa Utafiti wa Visumbufu vya Mimea na Udhibiti wa Chuo Kikuu cha Kilimo Cha Sokoine (SUA), Profesa Gration Rwegasira, alisema SUA imetoa wataalamu na kuwapeleka Kigoma, kuwafundisha wakulima na kuwaanzishia maabara ya utafiti wa tatizo hilo.

Profesa Rwegasira, alisema kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani (FAO), TPHPA, TARI, IITA, Plant Village Tanzania na wadau wengine, wanatengeneza mikakati ya kitaifa kukabili ugonjwa huo dhidi ya zao hilo muhimu katika maeneo mengi nchini na linaloliingizia taifa fedha za kigeni.

Ofisa Kilimo wa Shirika la Plant Village Tanzania, Joachim Gobanya, akizungumzia madhara ya ugonjwa huo mkoani Kigoma, alisema unashambulia migomba na vinaambukizwa kwa njia kuu mbili.

Alisema njia ya kwanza ni kupitia vipando vya migomba vyenye maambukizi ya virusi hivyo na njia ya pili ni kupitia wadudu mafuta wa migomba (APHIDS), ambao wana uwezo wa kufyonza utomvu kutoka kwenye migomba ambayo imeathirika na kupeleka kwenye migomba ambayo haijaathirika.




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Erasto Mhina akizungumza wakati akifungua kikao cha baraza la madiwani cha mapendekezo ya mpango wa bajeti ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, juzi. Kulia ni Ofisa Utumishi wilaya hiyo, Luth Mwelo, (wa pili kushoto) ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Salimu Sechambo na Kaimu Katibu wa CCM wilaya, Ajuaye Msigala. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# 'Samia anataka haki kwa wanyonge'

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Eliakim Maswi amesema lengo la Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ni kuhakikisha wananchi wanyonge wanapata haki.

Maswi aliyasema hayo juzi mkoani Kilimanjaro wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo uliofanyika viwanja vya stendi kuu ya mabasi ya mikoani mjini Moshi.

Alizitaja kazi zitakazofanyika wakati wa kampeni hiyo kuwa ni kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria, utawala bora, mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia, usimamizi wa mirathi na urithi, haki za ardhi na utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala, haki za binadamu na wajibu na ndoa.

Nyingine ni kutoa ushauri nasaha, huduma za kisaikolojia kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, msaada wa kisheria kwenye sehemu za vizuizi vya magerezani na vituo vya polisi, sehemu zenye mikusanyiko ya watu sokoni, minadani, shuleni na vyuoni.

Akitoa salamu zake, Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Wakili Boniface Mwabukusi alisema: "Wosia ndio namna pekee ya wewe ukifariki dunia kuendelea kuzungumza na kuelekeza unavyotaka mali zako zisimamiwe," alisema na kuonya kuwa:

"Unapokufa kibubu wajinga wote kwenye ukoo wako watakuja kunyang'anya mali za familia yako."

Alisema huduma ya msaada wa kisheria ni ibada kwa sababu ni suala la kushughulika na maisha ya watu ya kila siku, hivyo ni wakati wa kuifanya kazi hiyo kwa unyeyekevu na ukamilifu.

Katika hotuba yake, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alitangaza kiama kwa watu wanaokiuka sheria, haki za binadamu, kunyang'anya watu haki za mirathi, kusababisha migogoro ya ardhi na wanaoendeleza ukatili wa kijinsia kuwa watachukuliwa hatua kali.

Ndumbaro, alisema kampeni hiyo ni matokeo ya maono ya Rais Samia baada ya kubaini watu wengi wana kiu ya haki, jambo ambalo linathibitishwa na umati unaojitokeza kupata ushauri wa kisheria kila mahali inapofanyika nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema kampeni hiyo imekuja wakati mwafaka mkoani humo kutokana na watu wengi kuonyesha kiu ya kupata haki kwa kufuata sheria.

Awali akizungumza kwa niaba ya watakaotoa huduma za kisheria wakati wa kampeni hiyo, Mkurugenzi wa taasisi ya ushauri wa kisheria Mkoa wa Kilimanjaro ya KWIECO, Wakili Elizabeth Minde, alimpongeza Rais Samia kwa kuja na msaada huo wa kisheria na kuwa msaada mkubwa kwa wananchi hasa wa vijijini ambao hawakuwa na uwezo wa kulipia gharama kupata huduma za kisheria.

## VETA 'wamkuna' mkuu wa wilaya

**Na Hamida Kamchalla,** MKINGA

MKUU wa Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, Gilbert Kalima amekipongeza Chuo cha Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA) wilayani hapa kwa kuongeza thamani madini ya mawe na kuinua uchumi wa wananchi.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na kwa niaba ya mkuu huyo wa wilaya na Ofisa Tarafa ya Mkinga, Heugen Mkinga kwenye Maadhimisho ya Miaka 50 ya Ufundi Stadi na Miaka 30 ya VETA yanayofanyika katika viwanja vya chuo hicho.

Kalima, alisema uongozi wa chuo hicho unastahili pongezi kwa kukuza kipato cha wananchi kupitia madini hayo ya Tanga Stone baada ya kuyaongezea thamani na kupata soko la uhakika.

"Nipende kuupongeza uongozi wa chuo hiki kwa kuboresha kazi ambazo zinafanywa na wananchi hasa katika kuongeza thamani madini ya mawe ya Tanga Stone ambayo yanapatikana wilayani hapa.

Kwa kuongeza thamani, tunakwenda kuongeza kipato na kuwainua wananchi wa Mkinga ambao wanatapa tabu kuyatafuta mpaka kuyapata hayo mawe" alisema.

Alisisitiza kuwa kuna mambo ya kujivunia ambayo yanaonekana kupitia chuo hicho kwa kuzalisha vijana ambao ni msaada kwa jamii.


Alisema vijana wapatao 50 wamekuwa wakirudisha fadhila kwa kusaidia miradi ya jamii kwenye maeneo yao ikiwemo kuwaunganishia wananchi umeme bila tozo.

"Ndugu zangu, kwa Mkinga vijiji 85 vimesambaziwa umeme, bado vitongoji. Ni imani yangu wale vijana 50 wanaosomeshwa hapa watawasaidia wananchi kutatua kero walizokuwa wanazipata," alisema.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa wilaya, kabla chuo hicho hakijajengwa wilayani hapa, wananchi walikuwa wanafuata mafundi umeme Wilaya ya Tanga kwa ajili ya kuwaunganishia nishati hiyo.

"Lakini kwa sasa tuna imani wananchi watakwenda kuipata huduma hii karibu na kwa wakati," alisema.

Mkuu wa Chuo hicho, Kalvin Haule, alisema chuo chao kinatoa mafunzo ya ufundi wa umeme wa majumbani, uungaji, uchomeleaji vyuma, ushonaji na tekinolojia ya nguo.



# Mahakama za mwanzo kuendeshwa kidijitali

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA zote za Mwanzo Kanda ya Geita zinatarajia kuanza kutumia mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Machi 1, mwaka huu kwa ajili ya kurahisisha na kuboresha utendaji wake.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Geita, Kevin Mhina kwa mahakama hizo alilitoa juzi mjini hapa.

Jaji Mhina, alitoa agizo hilo kwa mahakama hizo wakati akifungua mdahalo wa mwaka mmoja wa Mahakama hiyo Kanda ya Geita.

Jaji Mhina, alisema mwaka jana walifanya majaribio ya matumizi ya mfumo huo katika Mahakama ya Mwanzo Nyankumbu na kuonyesha mafanikio kwa mahakimu kwa asilimia 80.

**"Mfumo wa TEHAMA unapunguza kufanya kazi, hakuna ya sababu ya kusema hiki hakionekani na inarahisisha ukaguzi wa majalada maana kila kitu kinaonekana hadharani," alisema Jaji Mhina.**

Alisema Machi 1 mwaka huu, mahakama hizo zitaanza kutumia TEHAMA na kuachana na matumizi ya makaratasi ili kupunguza matumizi ya fedha kwa kununua vifaa vya kufanyia kazi ofisini.

Alisifia TEHAMA kuwa unasaidia katika usimamizi wa kutoa haki kwa sababu kila kitu kinaonekana kwenye mfumo, kuokoa muda na ni rahisi.

"Mfumo wa TEHAMA unapunguza kufanya kazi, hakuna ya sababu ya kusema hiki hakionekani na inarahisisha ukaguzi wa majalada maana kila kitu kinaonekana hadharani," alisema Jaji Mhina.

Alisema mfumo huo umeokoa fedha nyingi mwaka jana ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya kununua kwa karatasi na kuhamishiwa kwenye matumizi mengine.

Alisema uwepo wa Mahakama Kuu Kanda ya Geita, pia umepunguza safari za wananchi kwenda Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza kupata huduma.



Mwenyekiti wa Kikundi cha Usikivu, Laurensia Lubigisa (kushoto), akitoa maelezo ya namna wanavyotengeneza unga wa lishe kwa Mkurugenzi wa Mifumo, Tathmini na Mawasiliano wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Makao Makuu, Japhet Boaz (wa tatu kushoto), alipotembelea kukagua miradi ya wanufaika wa ufadhili wa TASAF kupitia mradi wa kupunguza umaskini (OPEC), katika Manispaa ya Ilemela, jijini Mwanza, juzi. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Samia atunukiwa dhahabu kwa utendaji mzuri

**Na Halima Ikunji,** TABORA

UMOJA wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Tabora, umemtunuku Rais Samia Suluhu Hassan tuzo maalumu ya dhahabu kwa utendaji kazi na kupitishwa kupeperusha bendera ya chama hicho katika Uchaguzi Mkuu Oktoba mwaka huu.

Akizungumza juzi kwenye hafla ya kukabidhi tuzo hiyo, Mwenyekiti wa Umoja huo, Mwanne Mchemba, alisema wanawake wa Tabora wanamuunga mkono Samia kwa asilimia 100.

Mwanne, alisema hafla hiyo pia inalenga kumpongeza kiongozi huyo wa nchi kwa kuongeza mwaka mwingine wa kuzaliwa kwake, kukata keki na kukabidhi kadi maalumu ya 'Happy Birthday'.

Alisema katika hafla hiyo, pia walimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Mwinyi kwa utendaji wake na kupitishwa tena kutetea kiti cha urais kwenye uchaguzi huo utakaovishirikisha vyama vingi vya siasa nchini.

Vilevile, walimpongeza mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi.

"Hatuna mashaka na uteuzi wa viongozi hawa, kazi yetu ni moja tu kuwahamasisha akinamama wote wa Mkoa wa Tabora kujitokeza kwa wingi kuwapigia kura siku ya uchaguzi ili wapate kura za kishindo," alisema Mwanne.

Katibu wa UWT wa Mkoa huo, Rhoda Madaha, alisema wamejipanga kuhakikisha wanawake wote wa mkoa huo wanakuwa kitu kimoja na kuendeleza mshikamano wao hadi siku ya uchaguzi.

Rhoda, alifafanua kuwa tuzo hiyo waliyotoa kwa Rais Samia ni maalumu kwa ajili ya kupongeza juhudi za kuwaletea maendeleo Watanzania, Bara na Visiwani.

Akipokea tuzo hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa na Rais Samia, Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Mohamed Mtulyakwaku aliwashukuru na kueleza bayana kuwa kiongozi huyo ana dhamira ya dhati kuwainua kiuchumi.

Mtulyakwaku, alisema Samia ametoa fursa za mikopo kwa wanawake na wafanyabiashara wadogo ili kuwawezesha kiuchumi na kuchochea kasi ya maendeleo na kuwaomba waendelee kumuunga mkono kwa dhati.

# RC amuapisha DC kwa maagizo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amemuapisha Peter Masindi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu na kumuagiza kusimamia amani na kilimo cha Pamba wilayani humo.

Hafla hiyo ya kuapishwa kwa kiongozi huyo ilifanyika mapema wiki hii katika ukumbi wa mikutano wa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga na kuhudhuriwa na viongozi wa serikali wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Akizungumza baada ya kumuapisha Mkuu huyo wa Wilaya, Annamringi, alimsihi kutumia fursa ya kuaminiwa na Rais Samia kwa kuchapa kazi, kuwatumikia wananchi na kusimamia amani Kishapu.

Akizungumzia kuhusu pamba, alisema ni zao kuu la kiuchumi kwa wilaya hiyo na kuagiza kiongozi huyo, kutilia mkazo ili kuongeza mapato ndani ya wilaya.

"Nenda ufanye kazi kwa uaminifu kama ulivyoapa leo kwa maana wewe sio mgeni katika kazi," alisema Annamringi.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri wa mkoa huo kusimamia uandikishaji wanafunzi wa darasa la awali na la kwanza na wa kidato cha kwanza kuhakikisha wote wanaripoti shuleni kutokana na mahudhurio kuonekana siyo mazuri.

Aliwaasa wazazi kuwapeleka watoto wenye ulemavu shule na walimu kuwapokea na kuwaandikisha bila ya kujali hali zao.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama Mboni Mhita, akizungumza kwa niaba ya wakuu wa wilaya mkoani Shinyanga, alimkaribisha Masindi na kuahidi kumpatia ushirikiano katika utendaji wa kazi za serikali na wananchi.

Kwa upande wake Masindi, aliwaomba ushirikiano viongozi wa wilaya hiyo na mkoa huo ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

"Pale penye ushauri nipeni, kama mahali kuna tatizo mniambie ili turekebishe na kusafiri pamoja na maelekezo ambayo mkuu wa mkoa ameyatoa nitayafanyia kazi," alisema.

Aliye kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude ambaye amepangiwa kituo kingine na Rais Samia Suluhu Hassan, aliwashukuru viongozi wa Mkoa wa Shinyanga kwa kumpa ushirikiano wote wakati akitumikia wilaya hiyo na kuwakaribisha wilayani Arusha.




Ukurasa 13



Ukurasa 12

## Kinamama waajiriwa wenye watoto njiti, namna wanavyoteseka kazini wakiwa na 'vichanga'

BUFE
IJUMAA JANUARI 31, 2025
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Mara katika operesheni kuchanja ng'ombe hadi kuku wote wa mkoa

## • Mifugo mikubwa Mil. 7.4; kuku laki 5.5 kufikiwa

**Na Sabato Kasika**

MKOA wa Mara uko kwenye kampeni ya kuhamasisha wananchi, ili wajiandae kuchanja mifugo yao, kuwaepusha na magonjwa kama sotoka, yanayowashambulia na kuwaua.

Kampeni hiyo ilianza Januari 22 na imetangazwa kuendelea hadi mwanzoni mwa Februari , kisha itafuatia chanjo itakayotolewa kwa awamu mbili, kulingana na makundi ya mifugo yaliyopo.

Katibu Tawala Sehemu ya Uchumi na Uzalishaji, Musiba Nandiga, ameiambia Nipashe kwamba, ameshawasilisha hilo katika mkutano wa uzinduzi wa kampeni ya chanjo hiyo mjini Musoma hivi karibuni.

"Mkoa wetu una mifugo 4,745,411, ng'ombe ni 1,451,484. Miongoni mwa mifugo hiyo, mbuzi ni 707,442, kondoo 569,536, kuku 1,742,557 na wanyama wengine tulionao," anasema Nandiga.

Anafafanua kuwa, ng'ombe, mbuzi na kondoo watapatiwa chanjo kuanzia keshokutwa, Februari Mosi, hadi Machi 30 na kisha itafuata zamu ya kuku watakaochanjwa kuanzia Mei Mosi hadi 30 mwaka huu.

"Chanjo itakayotolewa kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo inahusisha magonjwa ya homa ya mapafu na sotoka, kwa upande wa kuku ni kwa ugonjwa mdondo," anasema.



Mifugo ikihudumiwa. **PICHA: MAKTABA**

Nandiga anasema, wananchi watatakiwa kuchangia fedha kidogo kwenye uchanjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo, huku chanjo ya kuku itatolewa bure.

Anafafanua kuwa, ni wajibu wa wananchi pamoja na kujitokeza na kushiriki katika kampeni hiyo ili mifugo yao ipatiwe chanjo stahiki ya kuzuia mlipuko wa magonjwa yanayoweza kudhuru mifugo yao.

### UMUHIMU WA CHANJO

Nandiga anataja faida za chanjo, zinasaidia kudhibiti magonjwa ya mifugo na kukuza soko la chanjo hizo zinazozalishwa nchini.

"Kwa sasa tunahamasisha kutumia chanjo zinazozalishwa ndani ya nchi yetu, zikiwamo za kutoka Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI), inayomilikiwa na serikali na chanjo zinazozalishwa na viwanda vinavyomilikiwa na sekta binafsi," anasema.

Anasema, ni muhimu kutumia chanjo zinazozalishwa nchini, kwani zinasaidia bidhaa hizo kuwa na soko la uhakika, pia kukuza ajira katika jamii.

Hapo anahimiza kwamba, chanjo za mifugo zinazozalishwa nchini, zitengenezwe katika mazingira rafiki na rahisi kutumiwa na wafugaji.

Anataja kuwapo magonjwa mbalimbali ya mifugo, na mengi yanadhibitiwa kwa njia ya chanjo, mahsusi akiutaja ugonjwa wa sotoka kwa mbuzi na kondoo, akinena ni ya gharama nafuu kudhibiti magonjwa ya wanyama.

"Tiba ni bei ghali endapo mnyama akiugua kwa kuwa wafugaji wamekuwa wakiingia gharama kubwa kutibu wanyama wao, ndio maana tunasisitiza chanjo, ili kudhibiti magonjwa ya wanyama kwani ni njia isiyokuwa na gharama kubwa," anasema.

Anasema ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo ni moja ya magonjwa yaliyo katika mkakati wa kutokomezwa duniani ifikapo mwaka 2030 na kwamba Tanzania imo katika orodha ya nchi zenye ugonjwa huo.

### FURSA KWA WANANCHI

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi, anawataka wananchi na wafugaji mkoani humo kuchangamkia fursa ya kampeni hiyo, kwa kujitokeza kwa wingi kuchanja mifugo yao.

Anasema serikali imewekeza katika kuwasaidia wananchi ili waweze kujiimarisha kiuchumi na kwamba, ni jukumu la kila mwananchi kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali katika kuboresha maisha.

"Wafugaji wote wa mkoani Mara kushiriki kampeni hii kwa kupokea elimu kutoka kwa wataalamu kuhusu chanjo ili mchanje mifugo yote kwa bei ya ruzuku," anasema Kanali Mtambi.

Anasema ni wajibu wa wakuu wa wilaya, viongozi wa halmashauri na wataalamu wa mifugo na wadau wa sekta ya mifugo kwenda kutoa elimu kwa wananchi na kuwahakikishia kuwa chanjo hizo ni salama na zote zimetengenezwa hapa nchini.

"Chanjo itakapoanza kutolewa, wataalamu na viongozi msimamie zoezi hilo ili zisitoroshwe kwenda nje ya nchi, tumejipanga kudhibiti hujuma hiyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa itakuwa makini kufuatilia utoaji wa chanjo hizo," anasema.

Rai yake anatamka, ni wataalamu wanaosimamia mifugo, kuona namna ya kuwatambua wafugaji nchini, ili ruzuku iliyotolewa na serikali iwanufaishe wafugaji Tanzania, ambao ndio walengwa wa kampeni hiyo.

### CHAMA WAFUGAJI

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Mrida Mshota, anasema chama hicho kimefurahishwa na hatua ya serikali ya kuanzishwa utaratibu wa kutoa ruzuku ya chanjo ya mifugo.

"Hii ni mara ya kwanza kwa nchi yetu kuwasaidia wafugaji kwa kuwapa chanjo za ruzuku. Kwa niaba ya wafugaji tunashukuru serikali kuwafikia wafugaji," anasema Mshota.

Anawaomba wakuu wa wilaya, viongozi wa halmashauri na wataalamu wa mifugo kushirikiana na vyama vya wafugaji kuwahamasisha wafugaji kushiriki kampeni ya utoaji wa chanjo hiyo ya ruzuku na kuwafafanulia wafugaji kuhusu madhara ya wao kutokuchanja mifugo yao.

BIASHARA

# Kinamama waajiriwa wenye watoto njiti, namna wanavyoteseka kazini wakiwa na 'vichanga'

## • Kuna 'sapoti' na maagizo ya juu, sheria yake bado!
## • ILO, WHO zilishaagiza; Mwanaharakati naye aanika

**Na Frank Monyo**

KUZALIWA mtoto, ni tukio la kipekee linaloleta furaha kubwa katika familia. Hata hivyo, hali inakuwa ngumu mtoto huyo anapozaliwa na matatizo kiafya, kama vile kuwa njiti (kazaliwa kabla ya muda wake wa kawaida).

Wazazi wa watoto njiti hukutana na changamoto kubwa hasa katika mazingira ya kazi, hasa katika taasisi za umma, kutokana na sera za kazi ambazo mara nyingi hazilengi mahitaji maalum ya wazazi hao.

Katika sehemu za kazi nyingi za umma na binafsi, mazingira hayazingatii changamoto wanazokutana nazo wazazi wa watoto njiti.

Baadhi ya changamoto hizo, ni ukosefu wa maeneo maalum kwa ajili ya kunyonyesha, kupumzika au kutoa maziwa ya akiba.

Wazazi wanachohitaji ni muda wa ziada kuwahudumia watoto njiti na mara nyingi hukutana na vikwazo, kwani taasisi nyingi hazina maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

Ni hali inayowafanya wazazi wahisi ama kutengwa au kudharauliwa, pale wanapohitaji kushughulikia mahitaji ya mtoto wao.

Mnamo Mei Mosi mwaka jana, Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango akatoa neno katika hilo likieleza ikiwa mfanyakazi atajifungua mtoto njiti, kipindi cha uangalizi maalum hakiwezi kuhesabiwa kama likizo ya uzazi.

Likizo ya uzazi huanza tu baada ya mtoto kumaliza kipindi cha uangalizi maalum, kulingana na tathmini ya madaktari.

Aidha, anasema mfanyakazi ataruhusiwa kutoka kazini kwa muda wa miezi sita baada ya likizo ya uzazi, ili kumwezesha kwenda kunyonyesha mtoto wake.

Dk. Mpango anasisitiza suala la afya ya mama na mtoto na hususan njiti ni kipaumbele kwa serikali ya Awamu ya Sita, ambayo kisheria kunatafsiriwa kuwapo likizo ya uzazi kwa wanawake wanaojifungua watoto kwa muda wa siku 84 ikiwa ni mtoto mmoja au siku 100 ikiwa ni zaidi ya mmoja.

Kiuhalisia, watoto njiti wanatajwa kuhitaji uangalizi wa karibu na kila mara, kwa sababu ya afya yao dhaifu, jambo linalowafanya wazazi kuwa na mahitaji maalum ya muda wa ziada au ruhusa za mara kwa mara.

Inatajwa mara nyingi waajiri hawaelewi hali hii inayosababisha wazazi kuhisi shinikizo la kutosheleza matarajio ya kazi huku wakihangaika na majukumu ya kifamilia.



Mzazi mwenye mtoto njiti akiwasilishiwa msaada kutoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa wodini, mkoani Kigoma.

Ofisi za umma katika mustakabali wa ustawi wa jamii kazini, nazo zaelezwa kuhitaji kuwa na maeneo maalum kwa ajili ya wazazi kunyonyesha au kupumzika, huku huduma za msaada wa kisaikolojia zikihitajika kwa wazazi wa watoto njiti.

Hiyo ni pamoja na kuimarisha miongozo ya kisheria, huku serikali ikiingiza vipengele vya ulinzi kwa wazazi wa watoto njiti katika sheria za ajira na sera za afya ili kuhakikisha haki zao zinazingatiwa kikamilifu.

**WHO NA ILO**

Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Kazi Duniani (ILO), pia zina miongozo inayolenga kulinda afya ya mama na mtoto, pamoja na haki za wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti.

**Sera na Miongozo ya WHO na ILO**

WHO, zinasisitiza umuhimu wa huduma bora kwa mama na mtoto, ikiwa ni pamoja na uangalizi maalum kwa watoto njiti.

Shirika hilo tayari lina miongozo inayopendekeza utoaji huduma za afya zinazozingatia mahitaji maalum ya watoto njiti na msaada kwa wazazi wao.

Kwa upande wake ILO, kuna Mkataba wa Ulinzi wa Uzazi (C183) wa mwaka 2000, unaopendekeza likizo ya uzazi ya angalau wiki 14 kwa wanawake wanaojifungua, pamoja na ulinzi wa ajira na haki za wafanyakazi wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua.

Ingawa mkataba huo hauzungumzi moja kwa moja kuhusu watoto njiti, unatoa msingi wa sera za kitaifa zinazoweza kuzingatia hali maalum kama hizi.

Inatajwa kwamba utekelezaji wake katika nchi wanachama wa WHO na ILO, zinahimizwa kuendeleza sera na sheria zinazolinda haki za wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti.



Mtoto njiti akihudumiwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**SURA YA TANZANIA**

Nchini Tanzania serikali imetangaza kuwa kipindi cha uangalizi maalum kwa watoto njiti hakitahesabiwa kama sehemu ya likizo ya uzazi na likizo hiyo itaanza tu pale mtoto atakapomaliza kipindi cha uangalizi maalum, kama itathibitishwa na madaktari.

Serikali pia inaendelea kuwekeza katika huduma za kihospitali kama vile ujenzi wa wodi maalum za uangalizi wa watoto njiti na kupeleka vifaa vya kusaidia watoto hata katika vituo vya kutoa huduma za afya, ikiwamo mashine za kusaidia kupumua.

**ELIMU NA UHAMASISHAJI**

Katika eneo kila tarehe 17 ya Novemba, kila mwaka, Tanzania huadhimisha Siku ya Watoto Njiti Duniani, kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wake, pia kuwajali watoto njiti na kuhakikisha wanapata haki zao.

Pia, Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM), inalenga kuhakikisha watoto wanapata malezi bora kuanzia utotoni, ikiwa ni pamoja na watoto njiti.

Dorice Mollel, Mkurugenzi wa asasi ya Dorice Mollel Foundation anasema: "Watoto njiti wanahitaji uangalizi wa kipekee na wazazi wao wanapaswa kuungwa mkono kwa kila hali.

"Kama jamii na waajiri, tunapaswa kuzingatia kwamba wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti wanahitaji si tu muda wa ziada kwa ajili ya kujali watoto wao, pia wanahitaji msaada wa kisaikolojia na huduma za afya zinazozingatia mahitaji maalum ya familia zao."

Anashauri kuwapo taasisi za umma na serikali zinazopaswa kuboresha sera, zitakazohakikisha kunakuwapo haki za wazazi kama vile kutoa likizo ya ziada kwa ajili ya uangalizi maalum wa mtoto na kuzingatia mazingira bora kazini.

Dorice anazitaja hizo zitawasaidia wafanyakazi kuwajibika kazini kwao kwa ufanisi, pasipo kuwa na shinikizo la kupuuza majukumu ya kifamilia yanayowakabili.

"Katika Dorice Mollel Foundation, tunaamini kuwa ulinzi wa haki za wafanyakazi, hasa wanawake wanaojifungua watoto njiti, ni sehemu muhimu ya maendeleo ya jamii.

"Kwa hiyo, tunaunga mkono juhudi zote zinazolenga kuboresha sera na huduma kwa wazazi wa watoto njiti." anasema Dorice, akiwa na maelezo ya ziada kuwa:

"Tunatambua changamoto kubwa wanazokutana nazo wazazi wa watoto njiti, hasa wanawake wafanyakazi.

"Ni muhimu kwamba wapewe muda wa kutosha na mazingira bora ya kufanya kazi, ili waweze kumhudumia mtoto wao na kujihusisha na majukumu ya kifamilia kwa usawa."

Kinachopendekezwa sasa kitaalamu ni kwamba, waajiri waweke sera zinazohusiana na uangalizi wa watoto njiti, ikiwamo kutoa maeneo maalum kwa ajili ya kunyonyesha na kupumzika.

Pia, kunatajwa haja ya kuwapo msaada wa kisaikolojia, ili kuwasaidia wafanyakazi watekeleze majukumu yao ya kifamilia.

Hicho ndicho kinachoifanya serikali, pia waajiri kuhitaji mabadiliko yanayohakikisha kuwa haki za wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti zinazingatiwa kikamilifu na kwa kufanya hivyo, tutakuwa na jamii yenye wafanyakazi wenye afya bora na familia imara.

**SAMIA NA NJITI**

Hulka ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, inajionyesha katika tukio la Julai mwaka juzi alipotoa shilingi milioni mbili kwa Mariam Mwakabungu (25), aliyejitolea kukumbatia watoto njiti katika Hospitali ya Rufani Mkoa Amana, jijini Dar es Salaam.

Mganga Mfawidhi wa Amana Dk. Bryson Kiwelu, akasema kuwa umma umeguswa na anachokifanya Mariam, akiwamo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuweka kipaumbele kwenye uboreshaji huduma za afya uzazi, mama na mtoto.

"Rais ametoa shilingi milioni mbili fedha taslimu kumpatia mama huyu, kwa kujitoa kwake na amewapongeza viongozi wa Wizara ya Afya na Amana kwa ubunifu huu na uthubutu wa mama huyu kuwa sehemu yetu," akatamka Dk. Kiwelu.

Ni hali iliyomtia hamasa kwa kuungawa mkono na Rais katika tendo hilo, hospitalini Amana, Mariam akieleza: "Sikutegemea nimeona kama ndoto Mimi nilikuwa najitolea tu nimeona kama jambo dogo kwangu niliona tu kama jambo la kawaida sikujua kama litafikia huku."

Hapo, mdau anayewaunga mkono watoto njiti, Mkurugenzi wa taasisi ya Dorice Mollel, akakisifu kitendo alichokifanya Mariam ni cha utu na ametoa mchango mkubwa kuokoa maisha ya watoto hao.

"Nampongeza sana Mariam, bado ni mdogo angeweza kufanya shughuli nyingine, lakini ameguswa kusaidia watoto hao njiti," anatamka Dorice.

Pia, Oktoba mwaka jana, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufani ya Amana, zikaandaa harambee kuchangia ukarabati na ujenzi wa majengo ya watoto njiti na wajawazito, fedha zinazopatikana kutumika kununua vifaa tiba.

Hafla hiyo ya uchangiaji iliyofanyika Oktoba 25, 2024 katika ukumbi wa Mlimani City Dar es Salaam, shilingi Bilioni 1.2 zilikusanywa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, akamuwakilisha Rais Dk. Samia.

Ndio kauli kama hiyo ya mwaka ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda, anayesema "Rais.Dk. Samia kaokoa maisha ya watoto njiti, kwa kuongeza Wodi ya Mama na Mtoto kwenye Hospitali ya Wilaya ya Bahi"


Hiyo inaungana na kauli ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, mwaka jana aliyetamka, kila mwaka nchini kuna watoto 200,000 wanaozaliwa.



Dorice Mollel, mkurugenzi wa taasisi inayopigania haki za watoto njiti na wazazi wao.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Udanganyifu, utoro, matusi katika mitihani vimezidi, ufumbuzi uje!






NA SABATO KASIKA

HIVI karibuni, Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) lilitangaza matokeo ya mtihani wa kidato cha nne. Tukaambiwa , huku matokeo ya wanafunzi 67 wakiwamo watano walioandika matusi yakifutwa.

Matokeo hayo ni ya mtihani uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana, kukiwapo idadi hiyo ya wanafunzi waliofutiwa matokeo yao kwa vitendo hivyo, ambavyo ni kinyume na utaratibu.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk Said Mohammed, anasema wanafunzi hao walioandika matusi ni tatizo la maadili na kwamba matusi hayakubaliki katika chumba cha mtihani na kila mahali.

Udanganyifu na kuandika matusi, ni kama vinatakiwa kuwa vya kawaida, kwani matokeo ya mtihani wa kidato hicho ya mwaka 2023, wanafunzi 102 walifutiwa kwa udanganyifu, watano kwa matusi.

Inatia mashaka kwamba nchi inaandaa wasomi wa aina gani kama wapo wanaotafuta kufaulu kwa udanganyifu huku wengine wakipoteza muda shuleni kujiandaa kuandika matusi kwenye karatasi za mitihani.

Yaani mwanafunzi anagharimiwa na wazazi au walezi ili apate elimu, lakini mwisho wa siku anaandika matusi katika katarasi za mitihani! Kama hapendi shule kwanini asikae tu nyumbani?

Mwanafunzi akishaingia sekondari anatarajiwa kuwa ni mtu ambaye ameanza kujitambua na kujua kile anachokifanya shuleni, lakini inasikitisha kuona bado wapo ambao hawajitambui hadi kupoteza muda wa miaka minne shuleni kwa maandalizi ya kuandika matusi.

Kama anavyosema Katibu Mkuu wa NECTA, hilo ni tatizo la maadili ambalo binafsi ninaamini linaanzia nyumbani, hasa kutokana na ukweli kwamba shule ya kwanza ya mwanafunzi ni wazazi au walezi.

Inawezekana hao wanaoandika matusi katika mitihani, ni wale ambao wazazi hawafuatilii maendeleo yao shuleni na hivyo wanakuwa huru kuhudhuria masomo shuleni au kushinda vijiweni.

Iwapo hakuna ufuatiliaji, ni rahisi wanafunzi kujiingiza katika makundi yasiyofaa na kujikuta wakiacha shule. Kwa mtindo huo, wanaweza kufika shuleni kuripoti kisha wakatoroka kwenda vijiweni.

Ninaamini mwanafunzi anayejitambua na anayejua kwa nini yupo shule, hawezi kusubiri kuandika matusi katika mitihani, badala yake anaelekeza nguvu katika masomo ili kwenye mitihani afanye vizuri.

Pamoja na hayo ya wanafunzi wanaoandika matusi, wale ambao wamekuwa wakisubiri kufanya udanganyifu ili wafaulu, wanajiandaa kuwa wasomi wasio na faida kwa familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Ingefaa, kila mwanafunzi atumie maarifa aliyopewa shuleni kwa muda wote wa miaka minne au sita kufanya mtihani badala ya kusubiri kufanya udanganyifu kwa lengo la kufaulu.

Sidhani kama ufaulu wa aina hiyo unaweza kuwa manufaa, kwani huku mbele anakokwenda anaweza kukosa msaada kwa udanganyifu na kujikuta akikwama kuendelea na elimu ya juu.

Hivyo, njia nzuri ya mwanafunzi kufaulu, ni kutumia maarifa ambayo amepewa na walimu wake ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kufaulu. Kufaulu kwa njia ya mkato, daima haina matokeo mazuri mbele.

Wakati kukiwapo changamoto hizo mbili za udanganyifu na kuandika matusi, ipo nyingine ya tatu katika elimu ambayo ni utoro unaofanywa na wanafunzi wa kidato cha kwanza kila mwaka.

Imekuwa ni kawaida kila mwaka wa masomo unapoanza, huwa kuna utoro mkubwa wa wanafunzi hao maeneo mbalimbali nchini, kitendo ambacho ni hatari kwa maendeleo ya elimu.

Kama ilivyo kwenye mitihani ya taifa kwa kuandika matusi au kufanya udanganyifu kila mwaka, ndivyo ilivyo kila mwaka kwa kidato cha kwanza kufanya utoro hadi serikali kuwasaka majumbani.

Mfano mmojawapo ni wa hivi karibuni ilipoelezwa kuwa wanafunzi zaidi ya 5,000 wa kidato cha kwanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime Vijijini mkoani Mara, walikuwa hawajaripoti katika shule walizopangiwa tangu zifunguliwe Januari 13 mwaka huu.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Simion Langoi, anasema hayo katika kikao cha hivi karibuni cha Baraza la Madiwani, kilichojadili bajeti ya halmashauri kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Inaelezwa kuwa wanafunzi 6,313 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu katika halmashauri hiyo, ni 1,233 pekee walioripoti shule walizopangiwa, huku wengine 5,080 wakiwa hawajulikani walipo.

Hiyo ni halmashauri moja tu, ukifanyika uchunguzi, ninaamini watoro wanaweza kuwa wengi zaidi, kwani imekuwa ni kawaida viongozi wa serikali sehemu mbalimbali nchini kufanya msako wa wanafunzi watoro kila mwaka na kuwarejesha shuleni.

Kwa kuwa matatizo hayo hujirudia kila mwaka, ninadhani ni wakati sasa umefika kwa serikali na wadau wake wa elimu kukaa pamoja na kuweka mikakati ya kuyamaliza ili kusaidia kuandaa vizuri taifa la kesho.

Ni kweli kuna jitihada mbalimbali ambazo serikali imekuwa ikifanya ikiwamo kufanya msako na kuwakamata wanafunzi watoro au wazazi wao, lakini tatizo linajirudia kila mwaka, hali ambayo inaonesha kuna haja ya kuja na mbinu nyingine zaidi zitakazokuwa na matokeo chanya.

UCHUMI

# Leo ikitimu siku marufuku kuni na mkaa kwa mamalishe, utekelezaji kiza kinene

**Na Beatrice Moses**

UTEKELEZAJI marufuku ya matumizi ya kuni na mkaa iliyotolewa na serikali kitaifa kwamba ifikapo Januari 31, 2025, iwe mwisho wa matumizi ya nishati hiyo. Huku ikiendeshwa kwa awamu.

Hiyo ni kauli ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kwa taasisi zote za umma na binafsi nchini zinazoandaa chakula na kulisha watu zaidi ya 100 kwa siku, kusitisha utumiaji nishati hizo kwa tarehe hiyo.

Marufuku hiyo pia ikawahusu watu wenye taasisi zinazoandaa kwa ajili ya watu zaidi ya 300 kwa siku, mamalishe na babalishe wanatakiwa kusitisha ifikapo Januari 31, 2025, ambayo ni leo.

Kurejea tulikotoka, mnamo Juni Mosi 2021, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitoa tamko la Wiki ya Mazingira Duniani na kuzielekeza taasisi, mashirika ya serikali na sekta binafsi, zianze kutumia nishati rafiki wa mazingira badala ya kuni na mkaa.

### UTEKELEZAJI WAKE

Kuna juhudi zimefanywa, zikiwamo manispaa tofauti kusambaza matangazo ya kusisitiza marufuku hiyo, pamoja na kugawa na kukopesha majiko na mitungi ya gesi kwa baadhi ya mamalishe na babalishe waliosajiliwa kwenye masoko rasmi.

Baadhi ya mama na babalishe, wameeleza hawana uwezo kununua majiko ya gesi, kutokana na kushindwa kumudu gharama zake.

Ofisa Mauzo wa kampuni moja inayouza gesi nchini, , Antony Martin, anasema kurahisisha utekelezaji wa matumizi ya nishati jadidifu, walitoa mkopo wa masharti nafuu wa majiko kwa baba na mama lishe.

"Tuliwakopesha kwa shilingi laki moja na hamsini jiko la gesi lenye sehemu mbili za kupikia, lakini ulipaji wa fedha umekuwa na changamoto," anasema Antony.

Said Juma, muuza chipsi na 'nyama choma' Mwenge wilayani Kinondoni, ameonesha mshangao akihoji marufuku hiyo, akisema.

"Sijui hiyo marufuku, sijui nitafanyaje maana mtaji wangu ni mdogo, kumudu kununua jiko la gesi ni mtihani kwangu, ngoja nisubiri tu itakavyokuwa."



Majiko ya mkaa wanayotumia baadhi ya mamalishe na babalishe, katika Soko la Simu 2000 lililopo wilayani Ubungo, Dar es Salaam. **PICHA : BEATRICE MOSES.**

Asha Omari, mamalishe katika Kituo cha Mawasiliano Simu 2000, Dar es Salaam, anasema alipewa jiko, lakini amelazimika kulipeleka nyumbani kwa kukosa usalama wa pa kupaweka.

"Tulipewa majiko watu kama 23 siku hiyo, lakini angalia mazingira yalivyo hapa siyo salama, nimelazimika kulihamishia nyumbani, hapa naendelea kupika kwa kutumia mkaa," amesema Asha.

Mariam Hemed maarufu 'Mariam Mdigo' anasema hana taarifa za kuwapo katazo la matumizi ya mkaa na kuni, pia hajapata jiko la gesi na mtaji wake ni mdogo.

Meneja Soko la Mawasiliano Simu 2000 Ahetwe Mkamba, anasema soko hilo lina mamalishe na babalishe 30 waliosajiliwa, baadhi yao tayari wamepewa majiko na mitungi ya gesi, kwa hatua za awali kuwawezesha kubadilika.

Ofisa Habari wa Manispaa ya Ubungo, Joina Nzali, anasema wamegawa mitungi 1200 zilizotolewa na wadau, mitungi 800 imegawanywa kwa mamalishe na babalishe waliosajiliwa.

"Tumetoa tangazo kuwakumbusha kuhusu utekelezaji wa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa mama na baba waliopo kwenye masoko ya manispaa yetu, tunaamini wamepata taarifa wameshajiandaa," anasema Joina.

### MTAALAMU MISITU

Mtaalam wa Misitu na Mazingira Dk. Felician Kilahama, pia Mkurugenzi mstaafu wa Misitu na Nyuki, anasema: "Hili ni jambo ambalo tulipaswa kuanza kulitekeleza mapema, ili kulinda misitu na mazingira kwa ujumla. Kikwazo kilikuwa ni miundombinu jinsi ya kufanikisha upatikanaji wa nishati hiyo kwa uhakika."

Anatahadharisha, upatikanaji nishati ukiwa wa gharama, wakati kipato cha wananchi kipo chini, utekelezaji mabadiliko itakuwa vigumu.

"Kuwe na ruzuku kama ikiwezekana, pia kuwe na uhakika wa kupatikana hiyo gesi, je ni ya asili hapa nchini au inaagizwa kutoka nje, hayo ni mambo yanayopaswa kuzingatiwa..." anasema.

Dk. Kilahama anafafanua changamoto ya utekelezaji ni jambo la wazi, kutokana na uhalisia wa mfumo wa maisha umezoeleka kama vile kupalia mkaa kwenye wali, inabidi kuwa makini na usimamizi wa misitu.

Katika andiko la Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) lililochapishwa Mei mwaka jana kwenye tovuti, inabainisha nishati na teknolojia sahihi inayotakiwa.

Nishati zinazopendekezwa zinatajwa kuwa zenye kiwango kidogo cha sumu, zinapotumika kwa usahihi, lengo ni kuhakikisha usalama uendelevu na upatikanaji rahisi wa nishati ya kupikia.

Hapo inatajwa kuokoa muda, kupunguza gharama, athari za kimazingira na kiafya kwa watumiaji, pia nyenzo muhimu kutekeleza makubaliano ya kitaifa na kimataifa kufikia mabadiliko ya tabianchi na kupunguza uzalishaji gesi joto.

Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, unatokana na hitaji la kuwa na mpango jumuishi kitaifa, kukabiliana na ongezeko la uharibifu wa mazingira pamoja na athari za kiafya, kiuchumi na kijamii, zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia.

"Kutokana na suala la nishati ya kupikia kuwa mtambuka, kumekuwa na changamoto ya utekelezaji wa mikakati ya kupunguza athari hizo.

"Tangu Tanzania ipate uhuru Mwaka 1961, haijawahi kuwa na mpango jumuishi wa kitaifa wa kupunguza matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia," inaelezwa.

### PICHA KITAIFA

Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 inataja azma ya kuongeza matumizi ya nishati tungamotaka na teknolojia yenye ufanisi kupikia, kuepuka uharibifu wa mazingira na matatizo ya kiafya yatokanayo na moshi.

Ni mkakati ulioandaliwa kutekeleza Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015. Inayonuia kuboresha matumizi ya nishati za kisasa za kupikia.

Pia, kuna matamko kitaifa kama:Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 yenye lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mazao, na huduma za misitu kwa kudumishwa eneo la kutosha chini ya usimamizi madhubuti.

Pia, Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007 inaelekeza uratibu bora na endelevu wa kuhifadhi, kutunza na kulinda mazingira kwa faida ya afya ya wanachi na vizazi vijavyo;

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mwanamke na Jinsia ya Mwaka 2000, nayo inalenga kutunza mazingira kwa kumpunguzia mwanamke mzigo wa kutafuta kuni na maji, ili kuwezesha kushiriki shughuli za kijamii na kiuchumi.

Kupitia uzoefu wa nchini India, sekta binafsi inashirikishwa kusambaza gesi asilia, serikali yake ikigawa maeneo maalumu kwa sekta hiyo kufanya usambazaji.

Vilevile, programu za kutoa ruzuku katika nishati safi ya kupikia kwa kaya za vipato vya chini, ni uzoefu uliochukuliwa, sasa serikali nchini imeandaa programu yenye lengo la kuchochea matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Hiyo inaendana na kuanzishwa viwanda vya bayogesi, kuwezesha kuzalisha nishati safi ya kupikia nchini.

Takwimu za Benki ya Dunia za Mwaka 2023, inawataja Watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia inaongezeka kiwango, kutoka asilimia 1.5 mwaka 2010 hadi asilimia 6.9 mwaka 2021.

Inaelezwa, kiwango hicho kiko chini ya wastani cha dunia, asilimia 71 kwa Mwaka 2021.

Mbali na gesi, nishati zingine zinazotumika kupikia nchini ni pamoja na kinyesi cha wanyama na mabaki ya mimea, kuni, mkaa, mafuta ya taa, mkaa mbadala, bayoethano, LPG, gesi asilia, bayogesi, umeme, majiko banifu na majiko ya nishati ya jua.

Kwa mujibu wa mkakati uitwao Cooking Energy Action Plan ya Mwaka 2022, asilimia 82 ya nishati kuu inayotumika nchini inatokana na tungamotaka (biomass).

Kwenye mapishi, asilimia 90 ya kaya nchini hutumia nishati kuni na mkaa kama nishati kuu ya kupikia ambapo matumizi ya kuni ni asilimia 63.5 na mkaa ni asilimia 26.2.

Asilimia 10 zilizobaki zinajumuisha asilimia 5.1 za LPG, asilimia 3 za umeme na asilimia 2.2 za nishati nyingine.

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18, nishati ya kuni yamekithiri hasa maeneo ya vijijini ambako asilimia 84.8 ya kaya hutumia nishati hiyo ikilinganishwa na maeneo ya mijini ambapo matumizi ni asilimia 17.4.





# Jaji Kiongozi ataka teknolojia itumike uchunguzi mashauri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) imetakiwa kutumia teknolojia ya kisasa kwa ajili ya kufanya uchunguzi kwenye mashauri yanayowasilishwa kwao.

Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Tanzania, Dk. Mustapher Siyani alitoa wito huo jana alipotembelea banda la taasisi hiyo, kwenye maonesho ya wiki ya sheria katika viwanja vya Nyerere Square.

Alisema TAKUKURU ni taasisi muhimu kwa jamii, hivyo inapaswa wajikite katika matumizi ya TEHAMA kwenye uchunguzi wa kesi mbalimbali zinazowafikia kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

Alisema matumizi ya TEHAMA kwenye utendaji kazi yanasaidia ikiwemo kurahisisha kazi mbalimbali ambazo wanapaswa kuzifanya kwa lengo la kutekeleza wajibu wao wa kila siku.

"Nawapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya katika maeneo mbalimbali hususani utoaji elimu, hivyo mjikite zaidi katika matumizi ya TEHAMA,",alisema Dk. Siyani.

Alisema dunia ya sasa inakwenda na teknolojia hivyo wanapaswa kuegemea huko ili kuboresha mazingira ya matumizi ya TEHAMA katika maeneo mbalimbali hapa nchini ili kurahisha utendaji kazi wao wa kila siku.

**"Nawapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya katika maeneo mbalimbali hususani utoaji elimu, hivyo mjikite zaidi katika matumizi ya TEHAMA," ,alisema Dk. Siyani.**

Aidha, aliwataka pia kupambana na kesi kubwa zenye viashiria vya rushwa ambavyo zinafikishwa mahakamani yakiwemo matukio mbalimbali ili kufikia malengo waliojiwekea kwenye Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050 ili taifa liwe miongoni mwa nchi inayodhibiti mianya ya rushwa.

Ofisa Uchunguzi kutoka TAKUKURU, Gabriella Gabriel alimshukuru Jaji Kiongozi kutokana na kutembelea banda lao, huku akisisitiza wanakwenda kufanyia kazi maoni waliyopewa katika wiki ya sheria.

Hata hivyo alisema tayari taasisi hiyo imeanza kutumia teknolojia kwa ajili ya utoaji elimu kwa jamii katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha jamii inapata uwelewa kuhusu mapambano dhidi ya rushwa.



Naibu Waziri wa Nishati, Judithi Kapinga (kushoto), akijadiliana jambo na Mbunge wa Jimbo la Makete, Festo Sanga (kulia) na Mbunge wa Hai, Saasisha Mafue walipokutana katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Neema yawaangukia wakulima, wafugaji, wavuvi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VYAMA vya ushirika vya wakulima, wafugaji, wavuvi na wajasiriamali walio nje ya mfumo wa fedha wanaotumia soko la ushirika wameletewa mwarobaini wa huduma za kifedha unaolenga kuleta ujumuishi na kuwaondoa kwenye mikopo umiza.

Akizungumza jana na waharfiri na waandishi wa habari jijini Dodoma, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Ushirika Tanzania, Godfrey Ng'urah, alisema wamedhamiria kuwafikia asilimia 78 ya Watanzania wasio na huduma za kibenki na wanatumia soko hilo.

Alisema watatumia rasilimali na fedha za wanahisa kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya kifedha hapa nchini kwa kuyagusa makundi hayo kupitia vyama hivyo ambavyo vipo 10,000 na vina wanachama zaidi ya milioni 10.

Alisema wameongea wigo wa bidhaa sokoni ikiwa ni pamoja na akaunti mahsusi kwa wajasiriamali, vijana na wanawake, mikopo ya bajaji na pikipiki kwa vijana, akaunti maalumu ya kilimo kwa wakulima isiyo na makato.

Alieleza kuwa mtaji umekuwa na kufikia Sh. bilioni 27.4 kwa mwaka 2024, sawa na ukuaji wa asilimia 640 ndani ya miaka minne tangu ilipoanzishwa mwaka 2020.

Alisema pia wamedhamiria kufika nchi nzima kutokana na kuwa ya kidigitali na itatumia ofisi za vyama vya ushirika kuunganisha mifumo ya kibenki ili kutoa huduma kwa Watanzania na hadi sasa ina matawi Moshi, Tandahimba, Dodoma na Tabora.

Naye, Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk.Benson Ndiege, alibainisha umuhimu wa Watanzania kuijua benki hiyo kwa kuwa itachagiza ushirika na kuongeza morali kwenye maeneo yote ya kiuchumi kwenye kilimo, uvuvi na ufugaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Benki hiyo, Prof. Gervas Machimu, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya kuhakikisha benki hiyo inaanzishwa na kuchangia Sh.bilioni tano na kuahidi kuhakikisha wanatoa mchango mkubwa kwenye ujumuishi wa huduma za kifedha.

# JWTZ kuanza kutoa huduma za afya ya akili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JESHI la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limesaini mkataba wa makubaliano ya utoaji huduma za afya ya akili na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe.

Mkurugenzi wa Tiba kutoka JWTZ, Brigedia Jenerali, Dk. Charles Mwanziva alisema hayo jana baada ya kusaini mkataba wa utoaji huduma za afya ya akili na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe.

Brigedia Jenerali Mwanziva alisema lengo kuu la mkataba huo ni kuwezesha wanajeshi kupata huduma mbalimbali za afya zinazopatikana hospitalini hapo.

"Mkataba huu utatusaidia sisi kama jeshi kupata huduma mbalimbali zikiwemo huduma za mazoezi ya viungo na utengamao," alisema Brigedia Jenerali Mwanziva

Alisema kuwa JWTZ litafaidika kwa kiasi kikubwa katika huduma za matibabu ya wagonjwa wa akili na hasa kwenye tiba maongezi (huduma za kisaikolojia).

"Leo tumefahamu pia kuwa siyo lazima kila mgonjwa anayekuja apewe dawa bali kuna tiba inaitwa ya maongezi ni tiba muhimu sana hasa kwetu wanajeshi itakayomrudisha mtu katika hali yake ya kawaida pindi apatapo changamoto", alisisitiza Brigedia Jenerali Mwanziva.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Paul Lawala alisema amefarijika kwa fursa ya JWTZ kushirikiana kwa karibu katika kutoa huduma za kibingwa na bobezi katika eneo la afya ya akili.

"Napenda kulipongeza jeshi kwa kuona umuhimu wa kushirikiana na sisi namna ya kuhudumia watu wao lengo ikiwa ni kuboresha ufanisi na utendaji kazi wa jeshi kuhakikisha watumishi wao wanakuwa imara katika afya zao za akili", alisema Dk. Lawala.

Dk. Lawala alisema mahitaji ya huduma ya afya ya akili katika jamii ni makubwa, hivyo wanaendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuwasaidia kuwa na uelewa juu ya magonjwa ya akili na dhana pana ya afya ya akili.



# Watu 680 waugua kipindupindu, 12 wafariki dunia

**Na Nebart Msokwa,**
CHUNYA

WATU 12 wamefariki dunia wilayani Chunya mkoani Mbeya kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu uliotokea wilayani humo kuanzia Oktoba mwaka jana mpaka sasa.

Kadhalika, katika kipindi hicho zaidi ya wananchi 680 wilayani humo wameugua ugonjwa huo.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Zuber Mzige alitoa taarifa hiyo juzi kwenye kikao cha baraza la madiwani cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo alisema ugonjwa huo umetokea kwa awamu mbili.

Alisema awamu ya kwanza mlipuko ulianza Oktoba ambapo watu zaidi ya 600 waliugua na kusababisha vifo vya watu 10 na kwamba awamu ya pili ilianza mwishoni mwa Desemba ambapo wagonjwa wamefikia 80 na vifo ni viwili.

Alisema kati ya vifo viwili vilivyotokea katika awamu ya pili kimoja kimetokea kwenye jamii na kimoja kilitokea kwenye moja ya kambi za kuwahifadhi wagonjwa wa mlipuko huo.

Alisema kata iliyoathirika zaidi na mlipuko huo ni Kata ya Kiwanja ambayo ni miongoni mwa kata ambazo kuna migodi mingi na wananchi hawana matumizi mazuri ya vyoo.

Alisema walipofanya uchunguzi walibaini kuwa waathirika wengi wa ugonjwa huo ni wachimbaji wa madini hasa kwenye Kata ya Kiwanja, Ifumbo, Itumbi na Makongolosi.

Alisema wagonjwa wanaougua ugonjwa huo wanatibiwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika Hospitali ya Wilaya, Kituo cha Afya Makongolosi, Zahanati ya Matundasi, Ifumbo na Kiwanja.

**"Watu wa kwenye migodi wameathirika zaidi kwa sababu hawana utamaduni mzuri wa kutumia miundombinu ya vyoo, kwahiyo tunaendelea kutoa elimu kwa kushirikiana**

"Watu wa kwenye migodi wameathirika zaidi kwa sababu hawana utamaduni mzuri wa kutumia miundombinu ya vyoo, kwahiyo tunaendelea kutoa elimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo watendaji na madiwani," alisema Mziga.

Alisema kwenye maeneo hayo ya migodi wachimbaji wamekuwa wakinywa maji ya mvua yaliyotwama kwenye madimbwi na kwamba maji hayo huwa yanakuwa na mchanganyiko na 'vinyesi' hali ambayo inasababisha mlipuko huo usiishe.

Dk. Mziga alisema wameshirikiana na wataalamu mbalimbali wakiwemo watu wa mamlaka ya maji na wengine kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hiyo kuchukua sampuli za maji na kupima ili kubaini hali ya tatizo.

Alisema vyanzo vingi vya maji walivyovipima walibaini kuwa kuna vimelea vya kipindupindu na hivyo wakaanza kuvitibu na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya vyoo na matumizi ya maji safi ya kunywa.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Ramadhan Shumbi aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya kuhamasisha wananchi kutumia vyoo kwa usahihi ili kutokomeza ugonjwa huo.

Alisema kipindupindu hakisababishwi na tatizo lingine zaidi ya uchafu na hivyo akasisitiza elimu ya usafi wa mazingira pia kuendelea kutolewa kwa wananchi hasa kwenye maeneo ya mikusanyiko.

Alisema katika wilaya hiyo kuna shughuli kuu mbili ambazo zinakusanya watu wengi ambazo ni uchimbaji wa dhahabu na kilimo cha tumbaku na hivyo akasisitiza maeneo hayo kuwekewa mkazo maal-



Mkurugenzi wa Benki ya Standard Chartered, Kenya na Afrika, Herman Kasekende (kushoto), akishiriki katika Mkutano wa Wakuu wa nchi za Afrika wa Nishati, jijini Dar es Salaam, mapema wiki hii. Katikati ni Mkuu wa Masuala ya Kampuni, Chapa na Masoko wa benki hiyo, Desideria Mwegelo na (kulia) ni Mkuu wa Kitengo cha Mashirika, Lewis Mlay. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maboksi, taka yatumika kutengeneza mkaa

**Na Halfani Chusi**

WANAFUNZI na wananchi wa Kipunguni zaidi ya 100 wamepewa mafunzo ya kutengeneza mkaa mbadala kwa kutumia maboksi na taka, lengo likiwa ni kuunga mkono ajenda ya serikali ya matumizi ya nishati safi na kuwakwamua kiuchumi.

Mafunzo hayo yalitolewa mwishoni mwa wiki na kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni kwa kushirikiano na taasisi ya Global Impact Transformation.

Akizungumza baaada ya kuendesha mafuno hayo, Kiongozi wa Sauti ya Jamiii Kipunguni, Seleman Bishagazi, alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuwakwamua kiuchumi ili na wao waweze kujiendeleza.

Alisema mkaa unaotokana na maboksi ni mzuri na unasaidia kupunguza gharama za maisha, huku akisisitiza hata utengenezaji wake ni rahisi.

Alifafanua kwamba mtu anaweza kutengeneza mkaa huo kwa nusu saa kisha akaukausha juani kwa siku tatu tayari kwa matumizi.

"Utunzaji wa mazingira ni jukumu la kila mtu, kwa sababu madhara yanapotokea hayachagui mtu wa kumuathiri, Hivyo ni vema tukashirikiana kwa pamoja kuunga mkono hizi juhudi za kibunifu" alisema Bishagazi.

Alisema mkaa huo hautoi moshi na ni salama, kwamba unaweza kutumika muda mrefu kuliko mkaa mwingine wa kawaida unaotokana na miti.

Hivyo, aliwashauri kinamama kurejeleza taka kuwa mkaa kunabana matumizi, kuwataka watumie mkaa mbadala kwa kuwa utengenezaji wake ni rahisi na unasaidia kutunza mazingira.

Mratibu Mkuu wa Shughuli za Global Impact Transformation, inayojihusisha kusaidia jamaii kupitia miradi mbalimbali, Hamphrey Ottaru alisema wamefika eneo la Kipunguni kuendesha mafunzo ya nishati mbadala ili kusaidia utunzaji wa mazingira.

Alisema pia wanasaidia kuwawezesha vijana kupitia miradi mbalimbali ya kijamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mwanafunzi wa kidato cha nne, Wini Josefu, alisema amepata elimu ya kutengeneza mkaa mbadala na kwamba kwa sasa anaweza kutengeneza akiwa nyumbani na akajipatia kipato kwa kuuza.

Mkazi wa Kipunguni, Kuruthumu Saidi alisema awali hakujua kwamba maboksi

# Watendaji kata, vijiji watengeneza risiti feki za mapato

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya watendaji wa kata na vijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wanadaiwa kutengeneza vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato visivyokuwa rasmi.

Imeelezwa kuwa vitabu hivyo wanavitumia kwenye ukusanyaji wa mapato hali ambayo inaweza kusababisha upotevu wa fedha za serikali.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, Maghela Ndimbo aliyasema hayo jana alipokuwa anatoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka jana.

Alisema watendaji hao wamekuwa wakivitumia vitabu hivyo visivyo rasmi kukusanya michango ya wananchi na hivyo kuwa na uwezekano wa kutokea kwa mianya ya rushwa inayoweza kuchangia upotevu wa mapato.

Alisema uchunguzi wa taasisi hiyo ulibaini kuwa watendaji hao wamekuwa wakinunua vitabu vya stakabadhi halali kutoka katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya hiyo lakini vinapokuwa vimekwisha wanajitengenezea vya kwao.

Alisema walibaini pia kuwa kuna uelewa mdogo miongoni mwa wananchi wa wilaya hiyo kuhusu aina ya vitabu vya stakabadhi vinavyostahili kutumika kwenye ukusanyaji wa mapato, hali ambayo inasababisha wasiendelee kuvipotea.

Alisema baada ya kubaini tatizo hilo maofisa wa TAKUKURU Wilaya ya Chunya, ilitisha kikao cha kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wa mapato ili wawe na uelewa utakaosaidia kuokoa mapato ambayo yanaweza yakapotea.

Aliwataja wadau walioshiriki kwenye kikao hicho cha kutoa elimu kuwa ni wananchi, maofisa biashara wa halmashauri na watoza ushuru.

Ndimbo alisema taasisi hiyo ilibaini kuwa katika Halmashauri ya Chunya kuna baadhi ya hospitali na vituo vya afya vimekuwa vikiwatoza wananchi fedha kwa ajili ya kupata huduma ya mama na mtoto.

Alisema vitendo hivyo ni kinyume na Sera ya Afya ambayo inaelekeza kuwa huduma hiyo inatakiwa kutolewa bila malipo na kwamba kitendo cha hospitali hizo kuwatoza kinasababisha manung'uniko.

Alisema taasisi hiyo itaendelea kutoa elimu kwa wananchi na kuwashirikisha katika kupinga vitendo vya rushwa kwa kutumia TAKUKURU rafiki.

# TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

## TANGAZO LA NAFASI 8,000 ZA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KATIKA FANI MBALIMBALI

1. Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini inayolenga kuwezesha nguvu kazi ya Taifa kupata ujuzi na stadi za kazi stahiki ili kumudu ushindani katika soko la ajira. Ofisi imeingia makubaliano na vyuo 52 vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi ambavyo vimesajiliwa na Mamlaka husika kutoa mafunzo katika fani mbalimbali zikijumuisha ubunifu wa Mitindo na Ushonaji Nguo, Ufundi Bomba, Uashi, Useremala, Uchomeleaji na uungaji vyuma, Upakaji rangi na maandishi ya alama, Upishi, Utengenezaji wa vipuri vya mitambo, Ufundi Magari na Mitambo, umeme wa majumbani na viwandani, Umeme wa Magari, Huduma za Hoteli na Utalii, Ukataji Madini na Ufundi vyuma.

2. Ofisi inapenda kuwatangazia vijana wa Kitanzania wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35 wanaopenda kujiunga na mafunzo katika mojawapo ya fani zilizoorodheshwa hapo chini wafike katika vyuo vya VETA vya Mikoa na Wilaya pamoja na vyuo vilivyoainishwa hapa chini ili kuchukua fomu ya kuomba kujiunga na mafunzo. Serikali itafadhili ada ya mafunzo kwa asilimia 100. Mwanafunzi / mzazi / mlezi atagharamia gharama nyingine zikijumuisha nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani. Mafunzo yataanza tarehe 03 Machi, 2025 na yatakua ya kutwa. Mwombaji anashauriwa kuomba mafunzo haya katika chuo kilicho katika Mkoa anaoishi.

3. Vituo vilivyokubalika na Serikali kutoa mafunzo hayo na fani zake vimeambatishwa.

4. Maombi yawasilishwe kuanzia tarehe 30 Januari, 2025 hadi 12 Februari, 2025 yakiambatana na nyaraka zifuatazo:

   i. Barua ya maombi ya mafunzo;
   ii. Nakala ya Cheti cha kuzaliwa;
   iii. Nakala ya Cheti cha elimu uliyohitimu ;
   iv. Kitambulisho cha uraia / kadi ya mpiga kura (Kwa wenye miaka 18 na kuendelea);
   v. Barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa/Kijiji anakoishi mwombaji; na
   vi. Picha nne za paspoti (ziandikwe majina matatu ya mwombaji kwa nyuma).

5. Sifa za kujiunga na mafunzo haya ni:
   i. Elimu ya msingi au zaidi kwa fani za ubunifu wa mitindo na ushonaji nguo, ufundi bomba, ujenzi, useremala, uchomeleaji na uungaji vyuma, upakaji rangi na maandishi ya alama;
   ii. Elimu ya kidato cha nne na kuendelea kwa fani nyingine zilizobaki zikijumuisha fani ya utengenezaji wa vipuri vya mitambo, ufundi magari, umeme wa majumbani na viwandani, umeme wa magari na umeme wa jua (solar);
   iii. Awe Mtanzania;
   iv. Awe na umri kati ya miaka 15 – 35; na
   v. Awe mwenye afya njema.

6. Vijana Wenye Ulemavu wanasisitizwa kuomba fursa hizi na watapewa kipaumbela katika nafasi za mafunzo haya;

7. Maombi yachukuliwe na kuwasilishwa kwenye vyuo vilivyo katika mkoa wako ambavyo vimekubaliwa na Serikali kutoa mafunzo haya.

8. Watakaokidhi vigezo na sifa tu ndio watakaochanguliwa

Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Ofisi (www.kazi.go.tz)

**IMETOLEWA NA:**

**KATIBU MKUU**
**30/01/2025**

NB: Fomu za maombi zinapatikana katika vyuo vyote vilivyopitishwa na Serikali kutoa mafunzo haya.

| NA. | MKOA | JINA LA CHUO | FANI ZILIZOKUBALIWA KUFUNDISHWA |
|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | Chuo cha Taifa cha Utalii Kampasi ya Arusha | Upishi |
| | | | Uokaji Mikate, keki |
| | | | Huduma ya Chakula na Vinywaji |
| | | | Mapokezi |
| | | | Huduma za Ndani na Utunzaji wa vyumba vya wageni |
| | | | Utalii na Usafirishaji |
| | | | Kuongoza Watalii |
| | | VETA Arusha VTC | Umeme wa Majumbani |
| | | | Ufundi Bomba |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi Magari |
| | | | Umeme wa magari |
| | | | Uungaji na Uchomeleaji vyuma |
| 2 | Dar es salaam | Don Bosco Vocational Training Centre - Oysterbay | Ufundi magari |
| | | | Useremala |
| | | | Upishi |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Uchongaji vipuri |
| | | | Umeme wa majumbani |
| | | | Umeme wa jua |
| | | | Ubunifu na ushonaji wa nguo |
| | | Chuo cha Marendeleo ya Wananchi Kigamboni | Umeme wa majumbani |
| | | | Umeme wa magari |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Ubunifu na ushonaji wa nguo |
| 3 | Dodoma | Don Bosco Technical Institute - Dodoma | Ufundi magari |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Upishi |
| | | | Huduma ya Chakula kula na vinywaji |
| | | | Uchongaji vipuri |
| | | | Umeme wa majumbani |
| | | | Umeme wa jua |
| | | | Ubunifu na ushonaji wa nguo |
| | | Institute of Heavy Equipment and Technology (IHET) | Ufundi wa mitambo |
| | | | Uendeshaji wa mitambo |
| | | | Umeme wa magari |
| | | | Ufundi magari |
| | | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu | Ubunifu na ushonaji wa nguo |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ufugaji wa wanyama na nyuki |
| 4 | Geita | Geita Vocational Training Centre | Ufundi umeme |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ubinifu na Ushonaji wa nguo |
| 5 | Iringa | Don Bosco Youth Training Centre, Iringa | Ufundi magari |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi umeme |
| | | Mafinga Lutheran VTC | Ufundi umeme |
| | | | Useremala |
| | | | Ufundi Magari |
| | | | Nishati Jadidika |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Upishi |
| | | | Ufundi Bomba |
| | | | Uchomeleaji na Uungaji Vyuma |
| 6 | Kagera | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ngara | Useremala |
| | | | Uashi |
| | | | Ubunifu na ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | Kashozi Home Craft Vocation Training Centre | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Upishi |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | VETA Karagwe | Ubinifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ufundi wa kielektroniki |
| | | | umeme wa magari |
| | | | Upishi |
| 7 | Katavi | VETA Mpanda VTC | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Uashi |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ufundi magari na mitambo |
| 8 | Kigoma | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibondo | Ufundi Umeme |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kasulu | Ufundi Umeme |
| | | | Uchomeleaji na Uungaji wa Vyuma |
| | | | Umeme wa Magari |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Uashi |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi Magari |
| 9 | Kilimanjaro | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mamtukuna | Ufundi magari |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ubunifu na ushonaji wa nguo |
| | | Marangu School of Tourism and Vocational Training | Kuongoza watalii |
| | | | Upishi |
| | | | Huduma za chakula na vinywaji |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ususi na urembo |
| | | | Mapokezi |
| | | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Same | Ufundi Magari |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Umeme wa Magari |
| | | | Upishi |
| 10 | Lindi | VETA Lindi RVTSC | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi magari na mitambo |
| | | | Ufundi umeme |
| | | | Umeme wa magari |
| | | | Upishi |
| | | | Huduma ya Chakula na vinywaji |
| | | VETA Ruangwa DVTC | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi magari |
| 11 | Manyara | VETA Manyara RVTSC | Ufundi magari |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi zana za kilimo na mitambo |
| 12 | Mara | Musoma Utalii Training college | Upishi |
| | | | Kuongoza Watalii |
| | | ST. Anthony Vocational Training Centre | Upishi |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ufundi wa magari |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Umeme wa magari |
| | | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tarime | Ufundi Umeme |
| | | | Ubunifu na ushonaji wa nguo |
| | | | Mifugo |
| | | | Useremala |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Ufundi bomba |
| 13 | Mbeya | Chuo cha Ufundi cha Magereza Ruanda | Seremala |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi rangi |
| | | | Uchomeleaji na Uunagji vyuma |
| | | Kyela Polytechnic College | Ufundi Umeme |
| | | | Useremala |
| | | | Ufundi Magari |
| | | | Uchomeleaji na Uungaji Vyuma |
| | | | Ususi na Urembo |
| | | | Upishi |
| | | | Ufundi Aluminium & PVC |
| | | | Uwekaji Marumaru na Vigae |
| | | VETA Busokelo DVTC | Useremala |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Ufundi wa Viyoyozi na Majokofu |
| | | | Ufundi umeme wa magari |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ufundi wa marumaru na terazo |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Ufundi vifaa vya aluminium na PVC |
| | | | Upambaji |
| | | | Upakaji rangi na maandishi ya alama |
| | | | Utengenezaji wa vipuri vya mitambo |
| 14 | Morogoro | Chuo cha Mafunzo Stadi - Garisa | Umeme wa Magari |
| | | | Ufundi wa Magari |
| | | | Saluni , Mapambo , Ususi na Urembo |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Mapishi na Ukarimu |
| | | Lakewood Training Institute | Kuongoza Watalii |
| | | | Ufundi Umeme |
| 15 | Mtwara | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mtawanya | Ufundi Umeme |
| | | | Uashi |
| | | | Uchomeleaji na Uungaji vyuma |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Masasi | Ufundi wa Magari |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Uashi |
| | | | Useremala |
| | | | Ufundi Umeme |
| 16 | Mwanza | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Malya | Ufundi bomba |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Uashi |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Sengerema | Ufundi meme |
| | | | Uchomeleaji na Uunagji vyuma |
| | | | Ufundi wa Magari |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi Bomba |
| | | | Umeme wa Magari |
| | | VETA Mwanza RVTSC | Ufundi Umeme |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Ufundi umeme wa magari |
| | | | Upishi |
| | | | Huduma ya chakula na vinywaji |
| | | | Usafi na utunzaji wa vyumba vya Wageni |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Upakaji rangi na uandishi wa alama |
| | | | Ukarabati wa mashine za kuchakata pamba |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Aluminium works |
| | | | Uashi |
| 17 | Pwani | VETA Pwani RVTSC | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | Vikindu Catholic Polytechnic College | Ufundi Umeme |
| | | | Upishi |
| | | | Umeme wa Magari |
| | | | Uundaji na Uungaji Vyuma |
| | | | Ufundi bomba na uunganishaji |
| | | | Ufundi viyoyozi wa majengo na magari |
| | | | Ufundi rangi na Uchoraji |
| | | | Ufundi wa Umeme wa Jua |
| | | | Uashi |
| 18 | Rukwa | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chala | Ufundi Umeme |
| | | | Ushonaji |
| | | | Umeme wa magari |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi magari |
| 19 | Ruvuma | Chuo cha Ufundi Stadi Mpapa | Useremala |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | Chipole Vocational Training Centre | Ufundi bomba |
| | | | Ufundi magari na mitambo |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Umeme wa majumbani na Viwandani |
| | | | Uashi |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | Peramiho Vocational Training Centre | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Uashi |
| | | | Useremala |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | Chuo cha Songea VTC | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Uashi |
| | | | uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Umeme wa magari |
| 20 | Shinyanga | Hill Forest College | Mapokezi |
| | | St. Francis de Sales Vocational Training Center | Ufundi Umeme |
| | | | Ufundi Bomba |
| | | | Ufundi Magari |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |
| | | | Saluni na mapambo |
| 21 | Singida | Chuo cha Ufundi na Marekebisho kwa watu wenye Ulemavu Sabasaba | Ususi na urembo |
| | | | Uokaji keki na mikate |
| | | | Umeme wa Majumbani |
| | | | Uchomeleaji |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | RC Mission Vocational Training Centre | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi wa magari na mitambo |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Umeme wa magari |
| 22 | Tabora | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Nzega | Ufundi Umeme |
| | | | Ufundi magari |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Useremala |
| | | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Sikonge | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | | Ufundi Bomba |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Uchomeleaji na Uungaji vyuma |
| | | Chuo cha Maendeleo ya Jamii Kaliua | Ufundi bomba |
| | | | Ufundi Umeme |
| 23 | Tanga | St. Patrick's Vocational Training Centre | Ufundi magari |
| | | | Umeme wa magari |
| | | | Ufundi Umeme |
| | | | Ubunifu na Ushonaji wa nguo |
| | | Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Handeni | Umeme wa majumbani |
| | | | Uashi |
| | | | Ufundi bomba |
| | | | Uchomeleaji na uungaji vyuma |





# Wadau wajadili washirika kupunguza misaada Afrika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAIMU Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Saidi Ali Mohammed amesema mamlaka za mapato Afrika Mashariki zinahitaji kuboresha zaidi usimamizi wa kodi kutokana na misaada ya washirika wa maendeleo duniani kupungua.

Mohammed, aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa 98 wa wadau wa kodi wa nchi hizo za Rwanda, Kenya, Sudan Kusini na Tanzania visiwani hapa.

Alisema lengo la kuwakutanisha wadau hao ni kujadili kupunguza utegemezi wa misaada kutoka kwa washirika hao, kukuza umiliki rasilimali na kuimarisha uwajibikaji wa kidemokrasia katika nchi hizo.

"Sote tunajua uhamasishaji wa mapato ni ufunguo wa maendeleo ya nchi. Mkutano huu umewaweka pamoja wasimamizi wa kodi Kanda ya Afrika Mashariki kujifunza kutoka kwa kila mmoja na kubadilishana uzoefu ambao utasaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato, ningependa kuwaomba, mtafakari jinsi tunavyoweza kuharakisha uhamasishaji wa mapato katika nchi zetu," alisema. Mohammed, alisema mamlaka hizo zinatakiwa kuwa na ubunifu na kupeleka mbinu rafiki kwa watumiaji ili iwe rahisi kukusanya kodi kutoka na wafanyabiashara na makundi mengine katika jamii. Alisema ni pia zinatakiwa kufanya utafiti wa kina na kushauri mikakati ya mageuzi ya kutekeleza, kurahisisha mifumo ya kodi na kukuza uchumi na maendeleo Afrika Mashariki.

**Aliwataka wakulima wa mpunga kuitunza miundombinu hiyo ili kuwawezesha kulima chakula kwa wingi na kuongeza kipato chao.**

Mohammed, alisema mkutano huo ambao pia utajadili njia mbadala za kudhibiti biashara za magendo nchini ni fursa nzuri ya kuimarisha Kiswahili kwa wageni kujifunzia lugha hiyo kwa sababu ni adhimu na kutambulika kimataifa.

Mwenyekiti wa kamati ya ufundi wa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki, Beatus Nchota, alisema katika jumuiya hiyo kuna ukwepaji kodi hususan kwa bidhaa za forodha za ndani.

Beatus, alisema mkutano huo pamoja na mambo mengine, utawasadia kutengeneza mikakati madhubuti kukusanya kodi hizo na nchi zao kupata mapato kwa ajili ya maendeleo katika jamii.

Akitolea mfano Kenya, alisema ni nchi iliyoanza kutoza kodi katika bidhaa zinazotengenezwa na pombe kali huku nchi nyingine zikiwa bado hazijaanza.

Mkurugenzi Utafiti na Mipango wa ZRA, Ahmed Haji Saadat, alisema kupitia mkutano huo watabadilishana uzoefu kwa wenzao na kupata jawabu ya changamoto zinazowakabili. "Kila nchi itawasilisha ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Disemba kwa kuangalia changamoto na njia ambazo wamezitatua," alisema Shaadat

Alisema kwa sasa ZRA inakabiliwa na changamoto ya uwajibikaji mdogo wa usajili kwa wafanyabiashara na baadhi kukwepa kulipa kodi licha ya kusajiliwa.



Mfanyakazi wa shamba la viungo la Zito, Amosi Salehe (Zito spaice farm), akitengeneza kofia kwa kutumia makuti, kwa ajili ya kuwapatia zawadi watalii wanaotembelea shamba hilo, eneo la Kizimbani, nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makala: Msichague wanaoeneza chuki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU wa Idara ya Itikadi, Mafunzo na Uenezi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amoss Makala amewataka wananchi kuwakataa viongozi wanaofanya siasa za chuki na uhasama visiwani hapa ili kundumisha amani na utulivu.

Makalla, alitoa wito huo katika mkutano wa hadhara uliofanyika Nungwi baada ya kuhitimisha ziara yake ya kichama Mkoa wa Kaskazini Unguja .

Aliwataka viongozi wa upinzani kuacha fitina na kupandikiza chuki kwa wananchi kwa lengo la kutafuta kura kwa sababu fitina zitasababisha uhasama miongoni mwao. Alisema kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, CCM itakuwa chama cha mfano kwa kufanya kampeni za kistaarabu bila ya kubeza watu, hivyo ni vyema wapinzani wakabadilika kuendana na siasa za uvumilivu.

"Hatuna Tanzania nyingine tunataka baada ya uchaguzi tubaki na Tanzania salama tutofautiane tu kiitikadi, tuimarishe na kulinda amani kabla, wakati na baada ya uchaguzi ili nchi iendelee kuwa na amani, " alisema.

Makala alitumia fursa hiyo kuwahimiza wananchi kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari la wapiga kura ili wapate haki ya kuchagua viongozi watakaowaletea maendeleo.

Akizungumzia ziara yake aliyoifanya katika mikoa miwili ya Pemba na Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema ameshuhudia uboreshaji Bandari ya Mkoani, ujenzi ya shule za ghorofa, hospitali za wilaya na jinsi Rais wa Zanzibar, Hussein Mwinyi alivyoibadili visiwa hivyo.

Alisema uwepo wa bandari hiyo utachochea kuongezeka kwa mzunguko wa fedha, mapato ya serikali, upatikanaji bidhaa haraka na kuongezeka kwa ajira.

Mwenyekiti wa CCM Kaskazini Unguja, Ali Ame Vuai, alisema duniani wananchi wanataka maendeleo, amani na utulivu na kuwataka wananchi kulinda tunu hizo.

Makala, alisema amani ya Tanzania imesababisha kuongezeka kwa watalii visiwani Zanzibar, hivyo ni vyema wanasiasa kuachana na siasa za chuki na uhasama ili kuidumisha.

## Kamati zatakiwa kusaidia wananchi kupata haki

**Na Mwandishi Wetu**

WAKILI wa Serikali wa Wizara ya Katiba na Sheria, Prosper Alexander amezitaka kamati za ulinzi na usalama ncnini kuwasaidia wananchi kupata haki zao.

Alexander alitoa wito huo kwenye mafunzo ya elimu ya uraia na utawala bora yanayoendeshwa na wizara hiyo kwa kamati hizo kuanzia ngazi ya vijiji hadi mikoa nchini na kuwajengea uwezo wa kwenda kusaidia wananchi kwenye maeneo yao.

Alisema mafunzo hayo yanayoendelea wilayani Newala Mkoa wa Mtwara, ni muhimu kuyatumia kwa vitendo mbele ya jamii wanapokutana na changamoto.

"Nawaomba mkatumie mafunzo haya kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kwa sababu wanahitaji kuipata elimu hiyo ili kutambua haki zao za msingi katika maeneo wanayotoka," alisema Alexander ambaye pia ni Mratibu wa Mafunzo ya Elimu ya Uraia na Utawala Bora wa Wizara hiyo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma na Sheria kwa Umma wa Wizara hiyo, Abrahiman Mshamu, alisema mafunzo hayo yatawasaidia wananchi kutambua Sheria Mama ya Tanzania. Mshamu, alisema mafunzo hayo yatatoa mwamko kwa mwanachi kushiriki kutoa maoni pale anapohitajika bila kuwa na wasiwasi.

"Wizara imeanza na mafunzo kwa watendaji wa kata ili wakawe mabalozi wazuri wa kutoa elimu kwa jamii kuhusu katiba na kubaini mapungufu," alisema. Mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala, Naomi Erick alisema anamini watendaji hao watakwenda kutoa elimu kwa wananchi ili kupambana na ukatili wa kijinsia.

HABARI KIMATAIFA

# HOFU VITA DRC KUENEA KIKANDA

## ● Kagame amtishia Ramaphosa ● EAC yaomba kuwepo suluhu



Waasi wa M23. **PICHA: MTANDAO**

**Goma,** DRC

HOFU imetanda kuhusu kutanuka kwa vita vinavyoendelea mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) baada ya Rwanda na Afrika Kusini kuingia katika mvutano mkali wa kidiplomasia.

Hali hiyo inatokana na Rais wa Rwanda, Paul Kagame kutoa onyo kali kwa Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, akisema Rwanda imejiandaa kwa mapambano iwapo kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo.

Hivi karibuni Ramaphosa, alionekana kukerwa baada ya wanajeshi tisa wa Afrika Kusini kuuawa wakati waasi wa M23 ambao wanaungwa mkono na Rwanda, kuuteka mji wa Goma.

Rais Kagame ilikuwa ikijibu maoni ya Rais Ramaphosa kuhusu kikosi cha wanajeshi wa Rwanda kusaidia M23 katika mapigano yanayoendelea mashariki mwa DRC.

Kauli hiyo ilionekana kumkasirisha Rais Kagame na kumkabili kwa maneno makali Rais Ramaphosa, jambo linalotishia kutanuka kwa mgogoroa huo.

Katika taarifa yake kupitia mtandao wa X, Rais Kagame alimshtumu kiongozi huyo wa Afrika Kusini kwa kupotosha mazungumzo yao ya faragha yaliyojikita kutatua hali tete mashariki mwa DRC.

Alisema Rais Ramaphosa katika mazungumzo yao hakuionya Rwanda kusaidia shughuli za kijeshi DRC lakini, badala yake aliomba msaada wa vifaa, umeme, chakula na maji kwa wanajeshi wa Afrika Kusini.

Hata hivyo, Kagame alisisitiza kwamba Afrika Kusini haina sifa ya kuwa mpatanishi katika vita hiyo na kuonya kama Afrika Kusini inataka mapambano, basi Rwanda itajibu ipasavyo.

Kwa upande mwingine, Rais wa DRC, Felix Tshisekedi, ameapa wanajeshi wake watapambana kwa jasho na damu ili kuyarejesha maeneo yaliyotwaliwa na waasi wa M23.

Mpaka jana kundi la waasi wa M23, limechukua maeneo mengi mashariki mwa DRC, ikiwemo mji mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini, wa Goma.

Katika hotuba yake ya kwanza tangu kutekwa kwa mji wa Goma, Rais Tshisekedi alisema jibu kali lililoratibiwa litatolewa dhidi ya magaidi na wafuasi wao.

Pia alikosoa jumuiya ya kimataifa kushindwa kufanya kitu katikati mwa hali mbaya ya usalama nchini humo.

"Kimya chenu na kutokufanya kitu ni dhihaka kwa DRC, mashambulizi ya wapiganaji wanaoungwa mkono na Rwanda yanaweza kusababisha kuongezeka kwa mgogoro katika kanda nzima ya Maziwa Makuu," alisema Rais Tshisekedi.

**EAC wazungumza**


Viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wametoa wito wa kuwepo kwa usitishwaji wa mapigano kati ya pande mbili zinazohasimiani nchini DRC.

Hata hivyo, walitilia mkazo serikali ya DRC kukaa meza moja na makundi yote, wakiwamo waasi wa M23 kutafuta suluhu ya kudumu.

Hata hivyo katika kikao hicho kilichoendeshwa kwa njia ya video, Rais wa DRC, Felix Tshisekedi hakuhudhiria, badala yake alifanya ziara ya ghafla nchini Angola kwa ajili ya kujadiliana na kiongozi wa nchi hiyo kuhusu mgogoro huo.

**Shinikizo kwa Rwanda**

Umoja wa Mataifa, Marekani, China, na Umoja wa Ulaya zimeitaka Rwanda kuondoa vikosi vyake vilivyoingia ndani ya DRC.



Hata hivyo, balozi wa Rwanda kwa ajili ya kanda ya Maziwa Makuu, Vincent Karega, aliiambia AFP kuwa harakati zinazofanywa na M23 zitaendelea.

Alisema inawezekana kwa wapiganaji hao kusonga mbele zaidi ya upande wa mashariki na hata kufika Kinshasa.

**Uporaji Goma**

Hali ya kiusalama katika mji wa Goma ilielezwa kuwa ni mbaya, huku makundi ya watu yamefanya uporaji katika maduka mengi ambayo wafanyabiashara wamekimbia.

Kulingana na shirika la habari la Ufaransa (AFO), kulionekana mistari mirefu ya wanajeshi wa serikali na wanamgambo wanaowaunga mkono wakitembezwa mitaani wakiwa wamefungwa vitambaa vyeupe kichwani.

Wacongo waandamana

Waandamanaji waliendelea kukusanyika mji mkuu wa nchi hiyo wa Kinshasa, kupinga vita hivyo huku wakichoma picha za rais wa Rwanda na kuchana bendera za Rwanda.

**Umuhimu wa Goma?**

Mji wa Goma uko karibu na Ziwa Kivu kwenye mpaka na Rwanda. Mji huo mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini lenye utajiri wa madini ni kitovu muhimu cha biashara, huduma ya kibinadamu na kituo cha ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa.

Jiji hilo pia lilikuwa kimbilio la raia wanaokimbia mapigano kati ya wapiganaji wa M23 na jeshi tangu kuzuka tena mwishoni mwa 2021.

"Suala la iwapo wanajeshi wa Rwanda kuunga mkono wapiganaji wa M23 ndani ya Goma halina mjadala ," alisema mkuu wa kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa Jean-Pierre Lacroix.

**Ukweli kuhusu M23**

Asili ya M23 inahusishwa na mivutano mingi ya kisiasa na kila wakati inabadilika. Kwa sasa kundi hilo la waasi ambalo linadai linapigania maslahi ya jamii ya Watutsi walio wachache mashariki mwa DRC.

Uasi wake wa kwanza ulianza muongo mmoja uliopita na ulimalizika kwa kundi hilo kupigwa na wanajeshi wa kimataifa na wapiganaji wake walipokonywa silaha na kwenda kuishi katika kambi nchini Uganda.

Miaka mitatu iliyopita, walianza kuondoka kambini wakidai mpango wa amani haukuheshimiwa na ndani ya miezi michache wakaanza kuteka maeneo.

Ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa - uliotumwa mara ya kwanza mwaka 1999, hauna mamlaka ya kufanya mashambulizi.

Vikosi viwili vya kikanda, kimoja cha Afrika Mashariki kiliondolewa na kile cha Kusini mwa Afrika (SADC) kimeshindwa kuwadhibiti M23.

Wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanaeleza kushindwa kwa vikosi hivyo inatoa mwanga kuhusu uwezo mkubwa walionao M23.

Kulingana na kundi la wataalamu wa Umoja wa Mataifa, uwezo wao unajumuisha mafunzo ya miezi mitano katika kambi kuu ya M23 iliyoko Tchanzu, eneo lenye milima, sio mbali na mpaka wa Rwanda.

Mafunzo hayo yanajumuisha kozi za nadharia na itikadi na kisha vitendo ikiwa ni pamoja na mbinu za vita,sheria za mapambano' na mbinu za msituni.

Inaelezwa kuwa maofisa wa kijeshi wa Rwanda mara nyingi walikuwepo kwenye kambi hiyo kutoa mafunzo kwa vijana waliletwa, waliojiunga kwa hiari na wengine walilazimishwa kujiunga kupitia operesheni maalumu ambapo machifu wanalazimika kutoa wapiganaji.

Wataalamu hao walisema Sultani Makenga, aliyepigana upande wa Kagame mwanzoni mwa miaka ya 1990 nchini Rwanda, ambaye sasa ni mkuu wa waasi wa M23, alihudhuria baadhi ya sherehe za wanajeshi 3,000 waliofuzu kati ya Septemba 25 na Oktoba 31.

Hata hivyo, msemaji wa serikali ya Rwanda, Yolande Makolo, hakujibu swali la iwapo wanajeshi wa Rwanda walikuwa katika kambi ya M23, lakini alikanusha tuhuma kuhusu kuajiriwa kwa watoto jeshini.

"Madai ya kuandikishwa watoto katika kambi ni ya upuuzi, ni vita vya wazi." Aliiambia BBC mwaka jana.

Hata hivyo, wataalamu wa Umoja wa Mataifa walieleza jinsi nguvu za M23 zilivyoongezeka tangu mwezi Mei, wakati huo ilipokuwa na wapiganaji karibu 3,000.

Wataalamu hao wanakadiria kuwa kati ya wanajeshi 3,000 na 4,000 wa jeshi la Rwanda wako ndani ya ardhi ya DRC. Walisema idadi hiyo inatokana na uthibitisho wa picha zilizopigwa kwa kutumia zisizo na rubani, rekodi za video, ushuhuda na ujasusi.

Wapiganaji waliokamatwa wa M23 walikiri kwamba wanajeshi wa Rwanda wanajulikana kuwa ni "friendly force" ikimaanisha vikosi rafiki.

# MORRISON AANIKA SIRI YEYE, NDUGUYE KUTUA KENGOLD

Na Adam Fungamwango

WINGA machachari kutoka Ghana, Bernard Morrison, amefunguka sababu iliyomfanya kujiunga na KenGold FC, si suala la kupewa ofa kubwa, bali ni kuanza upya maisha ya soka baada ya kutoka kwenye majeruhi ya muda mrefu.

Akizungumza mara baada ya kukamilika kwa Tamasha la Makarasha Day lililofanyika kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya juzi, ambalo lilikuwa ni rasmi kwa ajili ya kutambulisha wachezaji wapya, waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo, Morrison alisema amekaa kwa muda mrefu bila kucheza mpira baada ya kuumia wakati akiitumikia FAR Rabat ya Morocco.

Morisson alisema kufuatia hali hiyo, kwa sasa asingependa kusajiliwa na timu 'kubwa' ambazo zina mahitaji makubwa na zenye presha ya mashabiki.

"Mimi nimekuja hapa siyo kwa sababu ya pesa, au nimepata ofa nzuri, mimi nilikuwa majeruhi wa muda mrefu, niliumia wakati nipo FAR Rabat, sasa unapopona si vizuri kutua katika timu kubwa ambazo zina presha na mahitaji makubwa, kwa hiyo nimekuja hapa kama mtu anayeanza upya maisha.

Kitu muhimu ni kuisaidia KenGold kubaki kwenye ligi, siyo tumepata ofa nzuri sana," alisema Morisson.

Aliongeza ataangalia baada ya hapo, kama atakuwa fiti zaidi huko mbele ya safari anaweza kufanya uamuzi mwingine endapo atapata nafasi.

Alisema pamoja na yote hayo, lakini amekuja kwa nia ya kuibakisha KenGold Ligi Kuu kwa sababu ipo katika nafasi mbaya.

"Huu ni mpira tunaweza kufanya hivyo, ukiangalia timu imecheza mechi 16, lakini ina pointi sita tu, hivyo ni lazima tufanye kazi ya ziada kuisaidia, nyumbani tuna mechi kama nane hivi, hivyo tunajitahidi kushinda na nina imani tutabaki," winga huyo alisema.

Nyota huyo wa zamani wa Simba na Yanga, pia amemleta mdogo wake nchini, Ernest Morrison akiwa ni mmoja wa wachezaji waliotambulishwa rasmi kuvaa jezi ya KenGold hapo juzi.

"Nimemleta pia mdogo wangu kwa ajili ya kucheza Ligi Kuu Tanzania, unajua ligi ya hapa imeendelea sana na wachezaji wengi kutoka nje wanaitamani, sasa kama nina mdogo wangu ambaye ana uwezo kwa nini nisimwambie aje? Ndiyo kwanza anaanza maisha ya soka, kwa hiyo ni muhimu akianza sehemu ambayo ni bora na ina malengo na maendeleo, labda baada ya msimu huu anaweza kuondoka," aliongeza.

Kikosi cha KenGold kwa sasa kinajiandaa kuifuta Yanga kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Februari 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.



Winga mpya wa KenGold FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Mghana Bernard Morrison, akisalimia mashabiki wa timu hiyo wakati wa Tamasha la Makarasha lililofanyika kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya juzi. PICHA: MTANDAO

## Musonye ampongeza Karia CECAFA

Na Somoe Ng'itu

ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Nicholas Musonye, amempongeza Rais wa baraza hilo, Wallace Karia, kwa kuendesha mashindano mbalimbali katika ukanda huo kwa miaka mitatu mfululizo.

Musonye alisema kufanyika kwa mashindano ya vijana ya umri mbalimbali yameifanya CECAFA kufanya vyema kwenye michuano ya Afrika na msingi wa maendeleo hupatikana kupitia michuano hiyo.

"Nimeonya mashindano ya vijana ya U-15, U-17 na U-20, haya mashindano yanasaidia sana kukuza vipaji vya wachezaji wetu chipukizi, ili kuwaandaa wachezaji, ni lazima kuwa na mashindano kama haya, kila ninapoona mashindano yanafanyika, ninafarijika kwa sababu ninaona wanapita njia sahihi, ninampongeza sana Karia (Wallace) na Auka (Gecheo), ambaye ni Mtendaji Mkuu, wanafanya kazi nzuri sana," alisema Musonye.

Alisema yeye na Raisi wa zamani wa CECAFA, Leodegar Tenga, waliweka utamaduni wa kuweka misingi imara ya kupanga maendeleo kwa kufanya mikutano ambayo imesaidia kulinyanyua baraza hilo.

"Mimi na Tenga tuliongoza kwa miaka tisa, tunafurahi kuona wale tuliowaachia wanafanya vizuri, wanaendesha mikutano, wanajadili vizuri mipango ya maendeleo, hiki ni chama ambacho kinatusaidia kupanga mipango yetu," alisema Musonye.

Aliwataka pia wanachama wa CECAFA kulipa ada ambayo husaidia sekretarieti kujiendesha na kusimamia vyema shughuli za kila siku za baraza hilo lenye makao yake makuu nchini Kenya.

Musonye alialikwa katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa CECAFA uliofanyika Januari 22, mwaka huu Juba, nchini Sudan Kusini.

## Beki JKT Tanzania FC amfagilia nyota Azam

Na Adam Fungamwango

BEKI wa kushoto wa JKT Tanzania, David Brayson, amemtaja, Gibril Sillah wa Azam FC, ndiye winga hatari zaidi katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Brayson, alisema yeye binafsi anamkubali mchezaji huyo, lakini huwa wapendi kukutana naye kutokana na aina yake ya uchezaji ambao unasumbua.

"Kwa mtazamo wangu kama mchezaji, mimi ni beki wa pembeni, lakini katika mawinga wote niliowahi kuwaona, yule wa Azam FC, Sillah ni balaa. Binafsi ndiye winga wangu bora ninayemkubali kweli kweli kati ya wote hapa nchini. Na ndiye anayenipa tabu sana sitaki hata kukutana naye.

Ana ufundi sana mguuni, si mkimbiaji sana, hawezi kuondoka eneo la tukio bila mpira mpaka uwe mguuni, na akiwa nao ni balaa, yaani siku ukiona unakabana naye unajua kabisa kuwa leo kazi ipo," alisema Brayson.

Beki huyo ambaye aliichezea Yanga, msimu wa 2021, hadi 2023, alipojiunga na JKT Tanzania, kabla ya kujiunga na timu hizo, pia aliichezea Azam FC, ambayo kwa sasa Sillah yupo.

Sillah, mwenye miaka 26, ni raia wa Gambia, alisajiliwa na Azam Julai Mosi mwaka, 2023 akitokea Jeunesse Sportive de Soualem ya Morocco, ambako alikuwa akicheza kwa mkopo, klabu yake 'mama' ikiwa ni Raja Casablaca.

Kuhusu Ligi Kuu Tanzania Bara, Brayson, alisema imekuwa ngumu tangu mzunguko wa kwanza na anatarajiwa ushindani utaongezeka zaidi kwenye mzuguko wa pili, lakini wanajiandaa kwa ajili ya kukabiliana na ugumu huo.

"Tunajiandaa na mzunguko wa pili, walimu wetu wanatupa mazoezi ambayo tunaamini yatatuweka fiti ligi itakapoanza, naamini tutafanya vyema zaidi msimu huu kuliko uliopita kwa sababu tuna kikosi bora cha kufanya chochote kile kwenye mchezo wowote wa Ligi Kuu," alisema beki huyo.

JKT Tanzania inashika nafasi ya nane katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, ikiwa na pointi 19 baada ya kucheza michezo 16, ikishinda minne, sare saba na kupoteza mitano, ikifunga mabao 10 na kuruhusu magoli 12 kutinga kwenye wavu zake.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayoerejea tena kuanzia kesho huku Simba yenye pointi 40 ndio vinara.

## ZISIKUPITE

### VILLA: WATKINS HAUZWI

KLABU ya Aston Villa imekataa ofa ya pili ya Arsenal kumnunua mshambuliaji wake, Ollie Watkins, mwenye umri wa miaka 29, ambaye alikua shabiki wa washikabunduki hao. (***Mail***)

### RASHFORD MAMBO BADO

MANCHESTER United ipo kwenye mazungumzo ya muda na Barcelona kuhusu uhamisho wa mkopo wa mshambuliaji wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27, lakini kuna wasiwasi wa iwapo klabu hiyo ya Hispania itaweza kukamilisha dili kabla ya tarehe ya mwisho. (***Telegraph)***

### DIBLING AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Ujerumani, Bayern Munich na Borussia Dortmund zimeungana na Tottenham Hotspur katika mbio za kumsajili winga wa Southampton mwenye umri wa miaka 18, Tyler Dibling. (***Sun)***

### DURAN KUTUA AL NASSR

MSHAMBULIAJI wa Colombia, Jhon Duran, mwenye umri wa miaka 21 jana alitarajiwa kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu mjini London kabla ya pendekezo la euro milioni 77 pamoja na kuondoka Aston Villa kuhamia Al Nassr. (***Athletic***)

### TEL ANUKIA BAYERN

ARSENAL iko tayari kuipatia Bayern Munich ofa ya mshambuliaji wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 19, Mathys Tel, kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la Januari. (***Football Transfers)***

### NAPOLI YAMBANIA OSIMHEN

KLABU ya Napoli imekataa dau la euro milioni 65 kutoka Galatasaray kufanya uhamisho wa mkopo wa mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 26, kuwa wa kudumu. (***Corriere dello Sporty)***

### FITZGERALD KITAELEWEKA

NEWCASTLE United inatazamiwa kuzishinda klabu kadhaa za Ligi Kuu England katika mchakato wa kumsajili winga wa kimataifa wa timu ya vijana ya Jamhuri ya Ireland, Kyle Fitzgerald, kutoka Galway United mwenye umri wa miaka 18. (***Football Insider)***

### UNITED YAMBANI GARNACHO

NAPOLI imemwarifu winga wa Argentina mwenye umri wa miaka 20, Alejandro Garnacho, watakuwa tayari kujaribu kumsajili tena ikiwa Manchester United itapunguza bei yake. (***Fabrizio Romano)***


### GERRARD NJIA MOJA

STEVEN Gerrard ameripotiwa kuomba kuondoka kwenye klabu ya Ligi Kuu ya Saudi Aarabia ya Al Ettifaq baada ya miezi 18, kwa mujibu wa ripoti. (***Mirror)***

### CASADEI KUTUA TORINO

KLABU ya Torino ndio inayopewa nafasi kubwa ya kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea, Cesare Casadei, mwenye umri wa miaka 22. (***Gianlucadimarzio)***

# DONDOO ZA SOKA MAGA… A ULAYA



# AMORIM: RASHFORD ATAKIWA KUBADILIKA

**MANCHESTER,** England

**Lengo ni kupandisha kiwango chake ili kupata namba katika...**

KOCHA Mkuu wa Manchester United, Ruben Amorim, amemzungumzia tena Marcus Rashford, akiwaambia waandishi wa habari mshambuliaji huyo "lazima abadilike" kama atalazimika kurejea katika kikosi chake.

**Amorim amemtenga Rashford kwenye timu kwa mechi 11 mfululizo tangu waliposhinda mabao 2-1 dhidi ya Viktoria Plzen kwenye mechi ya michuano ya Ligi ya Europa iliyofanyika Desemba 12, mwaka jana akianza na ushindi wa dabi ya Manchester dhidi ya Manchester City.**

Baada ya United kushinda bao 1-0 dhidi ya Fulham Jumapili iliyopita, Amorim alisema ni afadhali amchague kocha wa makipa, Jorge Vital, mwenye umri wa miaka 63 kucheza kuliko Rashford (27), kutokana na kutokuwa na kiwango bora.

"Unaweza kuangalia timu yetu na kufikiria wasifu wa wachezaji. Sasa fikiria kipaji kama cha Rashford," alisema Amorim akiwaambia waandishi wa habari.

"Timu yetu inapaswa kuwa bora zaidi na Rashford pia. Lakini Rashford huyu, lazima abadilike.

"Iwapo atabadilika, tunamkaribisha zaidi kuweka kipaji chake hapa. Na tunakihitaji. Lakini kwa wakati huu, nadhani ni wazi tunapaswa kuweka viwango fulani. Tunamsubiri Marcus."

Kocha huyo wa Ureno aliendelea kukanusha kama kuna ugomvi wowote wa kibinafsi kati yake na mchezaji huyo, ambaye alisema mnamo Desemba alikuwa "tayari kwa changamoto mpya" baada ya kukosekana kwenye mechi dhidi ya City.

"Hilo ndilo jambo pekee. Ulijaribu kufanya kama kitu kibinafsi, sina chochote dhidi ya Marcus," alisema.

"Lazima nitengeneze sheria sawa kwa kila mtu na kwangu ni rahisi sana, huwa ni jibu sawa."

Rashford anaendelea kuhusishwa na kuondoka Old Trafford, huku ESPN ikiripoti wiki iliyopita wawakilishi wake walifanya mazungumzo ya ana kwa ana na Barcelona kuhusu uwezekano wa kuhama kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili wa majira haya ya baridi.




# RONALDO: MWANANGU ASEMA MBAPPE BORA KULIKO MIMI

**RIYADH,** Saudi Arabia

CRISTIANO Ronaldo anaweza kuwa ndio mchezaji bora wa wakati wote kwa mashabiki wengi duniani, lakini si kila mtu anayemkubali, kwa sababu nyota huyo wa Ureno amekiri mtoto wake wa kiume anampenda zaidi nyota wa Real Madrid, Kylian Mbappé.

Ronaldo alifunga mabao mawili katika ushindi mnono wa Al Nassr wa Ligi Kuu ya Saudia mwishoni mwa wiki, lakini hiyo haikutosha kumvutia mtoto wake wa miaka mitano mitano anayeitwa, Mateo.

Katika sehemu ya mahojiano yajayo na jarida la Hispania na La Sexta, Ronaldo alikiri nahodha huyo wa Ufaransa ndio kipenzi cha mwanaye.

"Mateo, anampenda sana Mbappé," alisema Ronaldo. "Wakati mwingine huniambia: 'Haya baba, Mbappé ni bora kuliko wewe,' na mimi hujibu kwa kusema: 'Hapana, mimi ni bora kuliko yeye, nimefunga mabao mengi zaidi.'"

Mbappé, ambaye anajulikana ni mshabiki mkubwa wa Ronaldo wakati wa utoto wake, ameanza kuiga baadhi ya mambo yake kule Bernabéu katika wiki za hivi karibuni baada ya uhamisho wake kutoka Paris Saint-Germain majira ya joto.

Baada ya hat trick yake dhidi ya Real Valladolid Jumamosi iliyopita, Mbappé sasa ana mabao 15 kwenye LaLiga, wa pili katika mbio za 'Pichichi' nyuma ya Robert Lewandowski wa Barcelona.

Ronaldo alifunga mabao 450 katika klabu hiyo ya Los Blancos kati ya mwaka 2009 na 2018.

# City yafuzu UEFA, Liverpool yaongoza

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City ilifuzu hatua ya mtoano ya mchujo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuifunga Club Brugge mabao 3-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Etihad juzi usiku.

Matokeo hayo yanamaanisha Kocha, Pep Guardiola, ameendeleza rekodi yake ya kusonga mbele kutoka hatua ya ufunguzi ya mashindano kila mwaka tangu kuanza kazi yake ya ukocha.



City walitawala mpira katika kipindi cha kwanza lakini walishindwa kutengeneza nafasi za wazi, ingawa Ilkay Gündogan aliweka mpira wavuni lakini alikuwa tayari ameotea.

Kikosi cha Guardiola kililazimisha bao hilo hadi kipindi cha pili, huku Mateo Kovacic, akiipa timu yake matumaini dakika ya 53 kwa shuti kali kutoka katikati ya Brugge na kumalizia vyema, kabla ya kazi ngumu ya Savinho kumfanya, Josko Gvardiol, kufunga bao la pili na Joel Ordóñez akajifunga mwenyewe.

Kampeni ya City barani Ulaya msimu huu imeshuhudia matukio kadhaa yasiyo ya kawaida, ikianza na ushindi wa mabao 4-1 ugenini dhidi ya Sporting CP iliyokuwa ikifundishwa na kocha wa sasa wa Manchester United, Ruben Amorim.

Kisha wakatupia uongozi wa mabao matatu ugenini kwa Feyenoord, wakaangukia kichapo cha 2-0 kutoka kwa Juventus na wakakubali manne dhidi ya Paris Saint-Germain Jumatano iliyopita na kuweka matumaini yao ya kusonga mbele katika shaka.

Liverpool walimaliza kileleni katika msimamo licha ya kufungwa mabao 3-2 na PSV Eindhoven huku Barcelona walio nafasi ya pili wakimaliza kwa sare ya magoli 2-2 na Atalanta.

Arsenal na Aston Villa zote zilishinda na kumaliza katika nafasi ya nane bora na kujihakikishia kusonga mbele kwa hatua ya 16, kama ilivyofanya Atlético Madrid.

Lautaro Martínez aliifungia Inter Milan hat trick walipoichabanga AS Monaco.

Real Madrid na Bayern Munich walishinda mechi zao za mwisho dhidi ya Brest na Slovan Bratislava, lakini wanakabiliwa na hatima sawa na City katika mchujo baada ya kuanza vibaya.

# Safari ya Nunez Saudia yakwama

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL haitakubali ofa kwa Darwin Nunez katika kipindi kilichobaki cha dirisha la usajili la Januari, ripoti zimesema, huku kukiwa na nia ya kutoka Ligi Kuu ya Saudi Arabia.

Nunez hajawa na mafanikio makubwa ya ufungaji mabao ambayo mashabiki wa Liverpool wangetarajia baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 85 kutoka Benfica, ambapo alifunga magoli 34 katika msimu wa 2021/22.

Raia huyo wa Uruguay amecheza mechi 29 hadi sasa msimu huu chini ya usimamizi wa Kocha, Arne Slot, lakini kimsingi ni mchezaji wa kikosi, akianza mechi saba pekee za Ligi Kuu.

Hata kwa hadhi hiyo, Nunez hana uwezekano wa kuondoka klabuni hapo siku zijazo.

Gazeti la The Athletic limeandika mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alikuwa akilengwa na Al Nassr, klabu ambayo nyota wa zamani wa Ligi Kuu England, Cristiano Ronaldo, Sadio Mane na Aymeric Laporte, waichezea.

Lakini msimamo wa Liverpool unaoripotiwa Nunez hauzwi katika kipindi hiki cha mwisho cha dirisha la majira ya baridi.

Nunez anatazamwa kama "sehemu muhimu" ya kikosi cha Liverpool, ingawa kunatarajiwa kuwa na "soko kubwa" kwa fowadi huyo katika majira ya joto ikiwa Wekundu hao wataamua kumuuza.



# HABARI MICHEZO

## Simba: Tutaizima Tabora United

INATOKA UKURASA 24

Tabora United itashuka uwanjani ikiwa na ahadi ya kupewa bonasi ya Sh. Milioni 50 kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora endapo itaifunga Simba katika mchezo huo.

Katika mechi ya keshokutwa, huenda Tabora United ikamkosa straika wake tegemeo, Heritier Makambo, ambaye anatumikia adhabu ya kuoneshwa kadi tatu za njano na winga, Yacouba Songne, ambaye ni majeruhi.

Pia kuna taarifa wachezaji wapya wa Tabora United waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo bado hawajapata vibali vya kufanya kazi nchini na kama mchakato huo hautakamilika, nyota hao pia wana hatihati ya kucheza mchezo huo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tabora United, Charles Obini, alisema kuelekea mechi dhidi ya Simba, yapo baadhi ya mambo wameyatatua na mengine yapo nje ya uwezo wao.

"Ni kweli, Makambo ana kadi tatu za njano, hawezi kucheza mchezo huo, Yacouba Songne yeye alikuwa majeruhi, ameanza mazoezi lakini kucheza kwake itategemea na kocha atakavyoona kama atakuwa amepona vizuri, hawezi kulazimisha kama hakuwa vyema.

Kuhusu wachezaji wapya, wote tayari tumewalipia vibali, tunachosubiri ni leseni tu, tukipata watacheza," Obini alisema.

Aliongeza kikosi chao kimejiandaa kucheza mechi hiyo dhidi ya Simba kama wanavyojiandaa na michezo mingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunajiandaa kama tunavyojiandaa na timu nyingine, hakuna mechi spesho eti kwa sababu tunacheza na Simba, maandalizi yetu ni yale yale tu kama tulivyojiandaa dhidi ya Yanga, KenGold, JKT Tanzania, Azam na timu nyingine, morali iko juu na tuna imani matokeo yatakuwa mazuri.

Vijana wanajiandaa vizuri, wachezaji wetu wageni nao wako vizuri, naamini mechi itakuwa nzuri kulingana na mipango yetu, sisi hatuna presha, tunajua mpira una matokeo matatu, tunaenda kucheza ili kupambana, litakalotokea sawa tu, hata tulipoenda kucheza dhidi ya Yanga hakuna aliyetegemea tutashinda, wenye presha ni Simba," Obini alisema.

Katika mechi iliyochezwa Agosti 17, mwaka jana, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Simba ikishinda mabao 3-0, yaliyofungwa na Che Fondoh Malone, Velentino Mashaka na Awesu Awesu Tabora United ilimkosa Makambo, Songne na wachezaji wengine ambao taratibu za usajili zilikuwa hazijakamilika.

Baada ya kusogezwa mbele kwa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), hadi Agosti 2, mwaka huu, Ligi Kuu Tanzania Bara inarejea rasmi kuanzia kesho kwa Yanga kuwakaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa KMC Complex.

# SAMATTA AFUNGUKA STARS IMEPANGWA KUNDI GUMU

**Na Somoe Ng'itu**

NAHODHA wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, amesema Tanzania imepangwa katika kundi gumu kwenye Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), ambazo zitafanyika mwaka huu nchini Morocco.

Taifa Stars imepangwa Kundi C katika fainali hizo zitakazofanyika kuanzia Desemba 21, mwaka huu hadi Januari 18, mwakani ikiwa pamoja na Uganda, Tunisia na Nigeria.

Stars itatupa karata yake ya kwanza Desemba 23, mwaka huu kwa kukutana na Nigeria halafu Desemba 27 itavaana na Uganda na itamaliza mechi za hatua ya makundi Desemba 30 kwa kukutana na Tunisia, mechi itakayofanyika kwenye Uwanja wa Prince Moulay ulioko jijini, Rabat.



Samatta aliliambia gazeti hili ili kufanya vizuri katika mashindano hayo, Stars inahitaji kupata maandalizi bora na mapema.

Nyota huyo alisema maandalizi sahihi yatasaidia kuwaimarisha wachezaji na kwenda Morocco wakiwa tayari na kamili kushindana.

"Nimefuatilia droo ya AFCON 2025 iliyofanyika Morocco, kundi letu ni gumu kama yalivyo makundi mengine, tunahitaji kufanya maandalizi ya kutosha kabla ya kuanza kwa mashindano," Samatta, mshambuliaji wa zamani wa Simba na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), alisema.

Nahodha huyo ameungana na Kocha Mkuu wa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco' ambaye ameshauri maandalizi ya timu hiyo yawahusishe Watanzania wote na si kuacha jukumu hilo kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

"Hili jambo si la mwalimu au benchi la ufundi, ni suala la kitaifa hasa pale katika uwezeshwaji wa kutekeleza mipango ya mwalimu, sisi kama benchi la ufundi tutakuja na programu yetu na naamini ikifuatwa vyema tutafanya vizuri kwenye fainali hizi," alisema Morocco.

Kabla ya kushiriki fainali hizo za AFCON, Taifa Stars imekata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika kuanzia Agosti 2 hadi 30, mwaka huu.

Tanzania, Kenya na Uganda ndio wenyeji wa fainali hizo za CHAN, ambazo awali zilitarajiwa kufanyika kuanzia mapema Februari, mwaka huu.




Wasanii wa ngoma ya asili ya kabila la kimasai wakicheza wakati wa mkutano wa Nishati wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dk. Tulia mgeni Bunge Bonanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika bonanza la Bunge litakalofanyika kesho kwa kushirikisha mashabiki wa timu za Simba na Yanga, jijini hapa.

Bonanza hilo lenye kauli mbiu 'Utani wetu, Umoja wetu' litahudhuriwa pia na viongozi, wanachama na mashabiki wa timu hizo kongwe nchini.

Akizungumza jijini hapa jana, Mwenyekiti wa bonanza, Festo Sanga, alisema pia watakuwa na mgeni maalum ambaye ni Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia huku na mwamuzi mstaafu wa FIFa, Othman Kazi.

Sanga alisema bonanza hilo litatumika kuhamasisha wananchi kufanya mazoezi kwa wingi kutokana na tishio kubwa la magonjwa yasiyoambukiza.

Aidha, alisema bonanza lengo lake ni kuleta mahusiano ya pamoja na taasisi mbalimbali zilizoko Dodoma zitashiriki ambazo zina mashabiki wa Simba na Yanga.

Meneja wa Benki ya Azania wa Tawi la Dodoma, ambao ndio wadhamini wakuu wa bonanza hilo, Liberia Peter, alisema michezo hiyo imeandaliwa kwa ajili ya kuhamasisha na kuimarisha afya za Watanzania.

## Yanga mguu sawa 'kuisulubu' Kagera

INATOKA UKURASA 24

kwa ajili ya kusaka namba, lakini sisi Yanga tumejiandaa kukabiliana na yote, tuko sawa kuivaa Kagera Sugar na kupata ushindi pia," alisema meneja huyo.

Yanga itaingia katika mchezo huu, ikiwa ni wiki moja tu baada ya kupata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Copco na kutinga hatua ya 32 Bora ya mashindano ya Kombe la FA.

Katika uwanja wa mazoezi jana, Kocha Mkuu, Sead Ramovic, alionekana kuwapa zaidi wachezaji wake mazoezi ya kurejesha utimamu wa mwili pamoja na kasi.

Mbali na Ikangalambo ambaye hakucheza mechi dhidi ya Copco, kutokana na kupatwa na homa ya ghafla, iliyomfanya asiwe kwenye mipango yake Ramovic, kesho huenda Israel Mwenda, ambaye alicheza mechi iliyopita kwa mara ya kwanza, na akatoa pasi mbili zilizozaa mabao, ataitumikia Yanga katika mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga yenye pointi 39 iko kwenye nafasi ya pili nyuma ya vinara, Simba yenye pointi 40.

KenGold FC ya jijini, Mbeya ambayo juzi iliwatambulisha nyota wake wapya akiwamo winga, Bernard Morrison, inaburuza mkia ikiwa na pointi sita kibindoni.

# Michezo

Ijumaa Januari 31, 2025

Nipashe



Amorim: Rashford atakiwa kubadilika UKURASA 21

# Simba: Tutaizima Tabora United FC

## ●●● Yatamba Mnyama si 'levo' yao, yaitaka isijikweze...

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wamesema wamejiandaa vyema kwenda 'kuizima' na 'kuondoa ukubwa' ambao Tabora United 'imejivika' kuelekea mechi ya ligi hiyo itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana kikosi chao kiko tayari kumaliza tambo za Tabora United kwa kuwaonesha wao bado ni timu ya daraja la kati.

**Ahmed alisema majigambo hayo yote yanayotokea sasa ni kwa sababu mabingwa watetezi, Yanga na Azam FC walikubali kufungwa na Tabora United, vinginevyo yasingekuwepo.**

Alisema kikosi chao kitaondoka jijini, Dar es Salaam kesho kuelekea Tabora tayari kwa mchezo huo ambao unasubiriwa kwa hamu na mashabiki na wadau wa soka nchini.

"Sisemi Tabora United ni timu mbaya, ila imekuwa na kiburi, mdomo na kujiamini kwa sababu ya kuzifunga Yanga na Azam, sasa tutakwenda kuwaonesha sisi sio hao ambao wamewafunga, sisi ni 'levo' nyingine kabisa, tunakwenda kuwaonesha wao ni timu ya daraja la kati na bado haina ukubwa huo inaojipa," alisema Ahmed.

Aliongeza wachezaji wa Simba wako imara kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi hiyo na kumaliza maneno, tambo na vijembe vinavyoendelea nje ya uwanja, kabla dakika 90 za kupambana dimbani.

INAENDELEA UK. 23



Winga wa Al Taraba, Simon Msuva, akijipanga kumiliki mpira katika mechi ya Ligi Kuu ya Iraq dhidi ya Karbala FC iliyochezwa hivi karibuni. Msuva, nyota wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), alifunga bao moja katika ushindi wa magoli 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga mguu sawa 'kuisulubu' Kagera

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wamesema wako tayari kuondoka na ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam ili kuendeleza mbio za kulibakisha taji hilo Jangwani.

Katika mchezo huo, wanachama na mashabiki wa Yanga wanatarajia kumwona kwa mara ya kwanza mchezaji wao mpya, Jonathan Ikangalombo, ambaye hakupata nafasi kwenye mchezo uliopita wa michuano ya Kombe la FA, dhidi ya Copco.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema ni muhimu kwao kushinda mchezo huo wa kwanza wa mzunguko wa pili ili kukiongezea nguvu kikosi chao kuelekea katika vita ya kutwaa ubingwa.

Akizungumza baada ya mazoezi ya jana asubuhi, Walter, alisema wanataka kuanza mzunguko wa pili kwa ushindi ili kuendeleza mbio za kubeba ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo msimu huu zimeonekana kuwa na kasi ya aina yake.

"Mchezo dhidi ya Kagera Sugar ni muhimu sana, kwa sababu malengo yetu yaliyosalia ni kubakisha taji letu la Ligi Kuu, Kombe la FA, kila kitu kinakwenda kwa mtiririko huu. Tumekuwa na maandalizi mazuri, kila kitu kinaenda sawa, kikosi kimetimia, kila mchezaji anaweza kuwa sehemu ya kikosi hicho, ukiondoa Yao Kouassi, ambaye amefanyiwa upasuaji.

Tunajua mchezo utakuwa mgumu kutokana na timu nyingi katika mzunguko huu zimefanya usajili, na kila mchezaji atajitahidi kucheza kwa nguvu ili kuwaaminisha walimu wao yuko sawa

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >